# Nipashe

Jumatano Septemba 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581068

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT
TZS. 1,031,243,893
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**Ajiua** madai ya kufumaniwa na mkewe akiwa na mwanafunzi

UKURASA 3


Mwiba wa tozo huenda ukaondoka kwenye vidonda

'Mama' amefariki lakini Mfalme ujngereza akumbushwa haya

siasa

Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

MFALME CHARLES III... Auchukua ufalme bila kujali yaliyopita

VIPORO MIGOGORO YA VYAMA

Ofisi ya Msajili yahofiwa pengine haiko huru, wadau wataka katiba kunusuru

UKURASA 11



# Mwigulu azidi kukabwa koo

• **CHADEMA** yataka ajiuzulu vinginevyo, yasema kuunda tume ni... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**ASKOFU RAMADHANI AFARIKI DUNIA DAR**

ASKOFU Mkuu Mstaafu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, John Ramadhani...

UKURASA WA 4

**AHUKUMIWA KUNYONGWA KWA KUMUUA MAMA MKWE**

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu...


UKURASA WA 8

**MABADILIKO SHERIA YA NDOA YAJA RASMI**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy...


## Anayeidai hospitali milioni 500/- atoa ushahidi

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akimpongeza Rais mpya wa Tano wa Jamhuri ya Kenya, Dk. William Samoei Ruto, baada ya kuapishwa katika Uwanja wa Kasarani jijini Nairobi jana. **PICHA: IKULU**

# Ruto aapishwa rasmi Rais wa Kenya, Samia apongeza uchaguzi wa amani

UKURASA 19


**MICHEZO** SIMBA BILA KANOUTE YAIPANIA PRISONS UK.24 **KABWELA** UK.18




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kulia), akimsikiliza Mkuu wa Idara ya Biashara za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo (wa pili kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo, wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), jijini Mbeya juzi. NMB ndio wadhamini wakuu wa mkutano huo wa siku tatu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA yataka Mwigulu ajiuzulu

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimekoleza moto kuhusu kilio cha tozo za miamala ya kielektroniki huku kikitaka Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba kuachia ngazi au atumbuliwe.

Katibu Mkuu wa CHADEMA amesema kutokana na suala hilo kuzidi kulalamikiwa na wananchi, ni vyema Dk. Nchemba akajiuzulu au Rais Samia Suluhu Hassan atengue uteuzi wa waziri huyo kwa kuwa ameshindwa kuchukua hatua sahihi za kisera kwa wakati sahihi kuhusu tozo.

Pia amesema waziri huyo anapaswa kusitisha mara moja kanuni za viwango vya tozo za miamala ya kibenki na kanuni nyingine kandamizi zinazohusu miamala ya kielektroniki.

Katika taarifa iliyotolewa jana, Mnyika alisema ni muhimu kwa serikali kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, ikiwamo kuachana na ununua magari ya kifahari ya kila taasisi, mamlaka za serikali za mitaa na watendaji wengine ambayo hayana umuhimu kwa taifa.

"Kuunda tume kwa ajili ya tozo ni matumizi mabaya ya fedha za umma, ni kuendelea kuwabebesha wananchi maumivu ya tozo kwa muda mrefu zaidi. Waziri wa Fedha (na Mipango) anapaswa kujiuzulu au Rais kutengua uteuzi wake," alisema Mnyika.

"Baada ya kusitisha, suala ambalo anaweza kufanya hata leo, upatikane ufumbuzi wa kudumu kwa kupeleka bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Fedha katika mkutano wa Bunge ulioanza leo (jana), ili kuepusha madhara ya muda mrefu na ya baadaye kwa nchi na wananchi kutokana na kasoro hizo za kisheria," alisema.

Mnyika alisema kuwapo kwa tozo hizo kumeathiri uchumi wa nchi pamoja na mzunguko wa fedha katika mfumo rasmi na hivyo kutishia uwapo wa uhai wa taasisi za kifedha.

"Watanzania walio wengi wanafanya uamuzi wa kuachana na utaratibu wa kuweka fedha au akiba kwenye mfumo rasmi kutokana na makato ya tozo ambazo zimeanzishwa na serikali baada ya sheria ya fedha kutungwa na bunge. Tozo hizi zinatozwa bila kujali kuwa wananchi walishalipia kodi ya mapato yao," alisema Mnyika.

Alitaja baadhi ya athari za tozo kwa wananchi kuwa ni pamoja na kuua ongezeko la watu kwenye mfumo rasmi wa kifedha jambo ambalo ni hatari kwa ukuaji wa uchumi kutokana na watu kuanza kutumia njia zisizo rasmi kuhifadhi fedha zao.

Alisema tozo hizo zinaathiri mishahara na pensheni ambazo zinapitia katika mfumo rasmi wa kibenki ambazo tayari zilishakatwa kodi, lakini zinatozwa tena kwenye mapato ambayo tayari yalishakatwa.

Athari nyingine alisema tozo zinapunguza nguvu za mtu mmoja mmoja katika kufanya manunuzi hususani wale ambao kipato chao hakiongezeki ikiwamo wastaafu.

"Wastaafu wanalazimika kulipa tozo kwenye mapato ambayo walishalipia kodi awali, huku ni kuwafanya wawe maskini na fukara zaidi,"alisema Mnyika na kuongeza kuwa tozo pia zinapunguza mzunguko wa fedha kwenye uchumi, hivyo kuathiri uzalishaji, na kwamba zinasababisha serikali kukosa mapato ya kodi.

"Mathalani kuna kampuni ambazo zimetangaza kupata hasara kutokana na wananchi kuamua kutokutumia mifumo rasmi ya kifedha. Tozo zisipodhibitiwa zitakuwa na athari kubwa kwenye taasisi za kifedha hasa benki kwa sababu wananchi wataamua kuwa na utaratibu wa kutunza fedha zao kwa mifumo ambayo sio rasmi, jambo ambalo litaudidimiza uchumi wa taifa," alisema Mnyika.

Alishauri kwamba ni vyema kuachana na utaratibu wa tozo na kurejea kwenye utaratibu wa awali pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwa serikali.

Pia alishauri kufanyike tathmini ya kina kujua faida na hasara za kuendelea na miradi mikubwa na mikataba ambayo serikali ya awamu ya sita imeiridhia ambayo haina msisimko wa kiuchumi na ambayo feza zote zinafanya manunuzi nje ya nchi na hivyo kusababisha mzunguko wa fedha kuwa mdogo.

Aidha, alishauri serikali kupunguza mikopo mikubwa ya kibiashara kwa ajili ya kujiendesha badala yake ikope kwa ajili ya miradi ya maendeleo na si kwa ajili ya miradi ambayo haisisimui uchumi wa taifa .

Mnyika alishauri ifanye uamuzi wa kuwezesha sekta binafsi katika kufanya biashara badala ya kuendelea kuendesha biashara ambazo inapata hasara kama vile miradi ya kuzalisha umeme na reli.

Pia ianzishe vyanzo vipya vya mapato kwenye sekta za uvuvi wa bahari kuu, kupanua wigo wa uzalishaji kwenye kilimo ili kujitosheleza kwa chakula pamoja na kuuza nje ya nchi.

## Anayeidai hospitali fidia mil. 500/- aanza kutoa ushahidi kortini

**Na Grace Gurisha**

MFANYAKAZI wa Wizara ya Kilimo, Florence Samwel, amedai mahakamani kuwa uchunguzi wa sampuli za tezi aliofanyiwa na Hospitali ya TMJ haukuzingatia weledi.

Pia amesema kulikuwa na uzembe kwa kupewa majibu yasiyo sahihi kuwa ana saratani.

Akitoa ushahidi wake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalira, alidai uchunguzi uliyofanywa TMJ ulikuwa na majibu tofauti na yaliyotolewa Hospitali ya Apollo kuhusu sampuli hizo yakionesha hana ugonjwa wa Rapillary Carcinoma of Thyroid, kama ilivyodaiwa na Hospitali ya TMJ.

Florence alidai hayo jana wakati akihojiwa na Wakili wa TMJ, Josephat Mabula, katika shauri la madai alilofungua dhidi ya hospitali hiyo, Hindu Mandal na Dk. Moirice Mavura, analodai fidia ya Sh. milioni 500.

Pia alidai sampuli zilizopimwa TMJ ndiyo zilizopimwa na Hospitali ya Apollo, kwa kuwa daktari aliyempa sampuli hizo alimtaka asizifungue na alifanya hivyo.

Kuhusu kiwango cha sampuli 15 zilizopimwa na Hospitali ya Apollo katika ripoti yake ya Januari 31, 2019, Florence alidai hajui jumla ya sampuli hizo kwa kuwa daktari aliyempa alimwelekeza asizifungue.

Florence alidai, hakubaliani na wakili huyo kuwa Hospitali ya Apollo ilitakiwa ijiridhishe kutokana na uchunguzi wake alioufanya na kwamba ana uhakika kuwa daktari wa TMJ hakuwa na weledi katika kazi yake.

Akiendelea kujibu maswali ya wakili huyo, Florence alidai kuwa upasuaji wa tezi aliyofanyiwa na Dk. Mavura, Julai 9, 2018 ulikuwa kimakosa, hakustahili kufanyiwa na pia katika ripoti ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ilieleza upasuaji huo ulikuwa ni hatarishi kwake.

Shauri hilo limeahirishwa hadi Oktoba 5, 2022 saa sita mchana kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Katika madai yake, Florence alisema Juni 27, 2018 alienda Hospitali ya Muhimbili na kufanyiwa uchunguzi wa koo ambako alielezwa amuone Dk. Mavura.

Alidai, baada ya kumwona Dk. Mavura, alimwelekeza aende Hospitali ya Hindu Mandal kutokana na kuwa na vifaa vya kisasa kwa ajili ya upasuaji.

Aliendelea kudai kuwa Julai 9, 2018, Dk. Mavura alimfanyia upasuaji katika koo lake na alitoa sampuli za tezi la kushoto zikapelekwa katika Hospitali ya TMJ kwa ajili ya uchunguzi ambayo ilitoa ripoti yake ikidai kuwa alikuwa na ugonjwa wa Rapillary Carcinoma of Thyroid.

Baada ya kukabidhiwa ripoti hiyo Dk. Mavura alimfanyia upasuaji wa pili na kuiondoa tezi iliyoambukizwa ugonjwa huo. Sampuli zilipelekwa katika Hospitali ya TMJ kwa ajili ya uchunguzi mwingine na ripoti ilionesha tezi hizo zipo sawa hazina ugonjwa wowote.

Florence alidai, alichukua majibu hayo hadi Hospitali ya Hindu Mandal na alipofika aliambiwa amekutwa na kansa ya Thyroid na anatakiwa aende katika Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa ajili ya kuanza matibabu ya mionzi.

Aliendelea kudai kuwa aliamua kuchukua uamuzi wa kwenda Hospitali ya Apollo kwa ajili ya uchunguzi zaidi na madaktari walibaini tezi ya kushoto inayosaidia kutengeneza homoni imeondolewa wakati alipofanyiwa upasuaji huo katika Hospitali ya Hindu Mandal.




Meneja Huduma za Jamii wa Benki ya NBC, Irene Peter (wa pili kushoto), akikabidhi sehemu ya taulo za kike katoni 125 kwa Meneja Mahusiano wa IPP, Nancy Mwanyika, jijini Dar es Salaam jana, zilizotolewa na benki hiyo ili kuchangia kampeni ya Namthamini, inayoendeshwa na East Africa TV na East Africa Radio, ambapo zitawasaidia wanafunzi wa kike wapatao 250 kwa mwaka mzima. Wengine ni Mtangazaji wa East Africa TV, Najma Paul (kushoto) na Mtangazaji wa East Africa Radio, Justine Kessy. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu John Ramadhani afariki dunia

**Na Waandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu Mstaafu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, John Ramadhani, amefariki dunia.

Kiongozi huyo aliyekuwa pia Askofu wa iliyokuwa Dayosisi ya Zanzibar na Tanga alifariki juzi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es Salaam alikokuwa amelazwa kwa ajili ya matibabu.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa Kanisa hilo, Mchungaji Canon Bethuel Mlula, ilisema kutokana na kifo hicho, Askofu Mkuu Dk. Maimbo Mndolwa, anasikitika kutangaza kifo hicho.

Alisema kuwa Askofu Mkuu Ramadhani (Pichani) alizaliwa Zanzibar Agosti 1, 1932 akiwa mtoto wa Mwalimu Augustino Ramadhani na Bibi Magreth Ramadhani.



Alihitimu shahada katika Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki na baadaye Chuo cha Queens Birmingham na Chuo Kikuu cha Birmingham nchini Uingereza.

"Aliwahi kuwa Mkuu wa Chuo cha Ualimu cha St. Andrew Korogwe kuanzia 1967 hadi 1969, alipata daraja la ukasisi mwaka wa 1976 huko Zanzibar. Alikuwa mkuu wa Chuo cha Theolojia cha Mtakatifu Marko, jijini Dar es Salaam kuanzia mwaka 1977 hadi 1979," alisema.

Askofu, Ramadhani aliwekwa wakfu kuwa Askofu wa Dayosisi ya Zanzibar na Tanga katika Kanisa la Mtakatifu Augustino, Chumbageni, Januari 27, 1980 akimfuatia Askofu Yohana Jumaa aliyakuwa katika nafasi hiyo mwaka 1968 hadi 1980.

"John Ramadhani alikuwa Askofu wa Dayosisi ya Zanzibar na Tanga hadi mwaka 2000 na alikuwa Askofu mwangalizi wa Dayosisi ya Zanzibar mwaka 2001 hadi 2002 kabla ya kuwekwa wakfu kwa Askofu Douglas mwaka 2002," alisema.

Askofu Ramadhani aliwekwa kitini kuwa Askofu Mkuu wa Kanisa Aglikana Tanzania 1984 na ambapo alihudumu hadi mwaka 1998 alipostaafu na nafasi yake kuchukuliwa na Askofu Donald Mtetemela wa Dayosisi ya Ruaha, Iringa mwaka 1998 hadi 2008.

Aliongeza kuwa kabla ya kuwa Askofu Mkuu wa Kanisa Aglikana Tanzania Askofu Ramadhani alikuwa mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Askofu Ramadhani amehudumu katika nyadhifa mbalimbali na amehusika kutoa mchango mkubwa sana kwa kanisa na jamii. Kanisa tutaendelea kuyaenzi mema yote aliyoyafanya baba Askofu Ramadhani katika kipindi cha uhai wake," alisema Mlula.

Kutokana na kifo hicho, Canon Mlula alisema kanisa linatoa pole kwa familia ya baba Askofu Ramadhani, wahudumu na Wakristo wote wa Dayosisi ya Zanzibar na kanisa lote kwa ujumla kwa msiba huo mkubwa. Alisema taratibu za mazishi zinafanyika kwa kushirikiana na familia.

Askofu Ramadhani alikuwa Askofu Mkuu wa Tatu wa Kanisa la Anglikana Tanzania akitanguliwa na John Sepeku (1970 hadi 1978), Mussa Kahurananga (1979- 1983). Wengine walioshika nafasi hiyo ni Mtetemela (1998-2008), Dk. Valentino Mokiwa (2008-2013), Dk. Jacob chimeledya (2013- 2018) na Dk. Maimbo Mndolwa 2018 hadi sasa.

**•Imeandikwa na Paul Mabeja, DODOMA, na Victoria Mgodomi (TUDARCo), DAR.**

# Ajiua kwa madai ya kufumaniwa na mkewe akiwa na mwanafunzi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKAZI wa Mtaa wa Kanisa B, Ludewa mkoani Njombe, John Mhagama (42), amejiua kwa kunywa sumu baada ya kufumaniwa na mke wake akiwa kwenye mazungumzo ya kimapenzi na mwanafunzi wa kidato cha kwanza.

Imeelezwa kuwa Mhagama kila ilipokuwa inafika majira ya jioni, alikuwa akienda kununua mkaa wa matumizi ya nyumbani kumbe nia yake ilikuwa kwenda kukutana na binti huyo na kumpatia pesa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issah, alisema siku ya tukio Mhagama alienda kununua mkaa kama kawaida yake huku mkewe akimfuatilia kwa nyuma na kumwona akizungumza na binti huyo (jina linahifadhiwa) na kumpa Sh. 5,000 huku akimbembeleza kumkubalia kuwa na uhusiano wa kimapenzi kwa kuwa alikuwa akichukua pesa zake pasipo kumtimizia.

Wakiwa katika mazungumzo hayo, Kamanda Issa alisema mkewe alijitokeza na kuanza kumlaumu mumewe kwa kitendo alichofanya na kwa hasira Mhagama alimpiga mkewe kisha kurudi zake nyumbani.

Kwa mujibu wa maelezo ya mkewe huyo, Issah alisema kutokana na hasira alizokuwa nazo mumewe, hivyo hakutaka kurejea nyumbani kwa muda ule lakini baada ya muda kidogo alipigiwa simu na shangazi wa marehemu akimjulisha kuwa Mhagama ana hali mbaya ndipo alipokwenda nyumbani na kumpeleka hospitalini ambako mauti yalimkuta.

Katika tukio lingine, Razalius Kufabasi (50) mkazi wa kijiji cha Lusala wilayani Ludewa, anashikiliwa na polisi kwa madai ya kumpiga na tofali la kuchoma kwenye paji la uso Linus Mtega (52) na kumsababishia kifo.

Kamanda Issah alisema siku ya tukio kulikuwa na ujenzi wa makabuli na majira ya usiku watu walikuwa wakiburudika kwa muziki na Mtega alikuwa amemkumbatia mke wa Kufabasi huku wakicheza pamoja kitu ambacho kilimpa wivu mzee huyo na kuamua kuchukua tofali na kumpiga nalo kwenye paji la uso.

Kamanda Issah alisema Mtega alichanika paji la uso na kupelekwa katika Kituo cha Afya cha Mlangali lakini hakupona na kufikiwa na umauti.

Issa alisemka kutokana na kutenda kitendo hicho, Kufabasi alijaribu kutoroka lakini alitiwa nguvuni na Jeshi la Polisi.

Kamanda Issa amelaani vikali tabia hizo huku akiitaka jamii kuacha wivu uliopitiliza kwa kuwa yanapotokea mauaji kama haya, familia na watoto ndizo huteseka.


Ujamaa Community Resource Team
EMPOWERMENT JUSTICE STEWARDSHIP
PO Box 15111, Arusha, Tanzania
www.ujamaa-crt.org

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI

SHIRIKA LA UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM NI SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI LINALOJISHUGHULISHA NA KUJENGA UWEZO WA JAMII KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA, ARDHI NA MAZINGIRA KATIKA MKOA WA ARUSHA.

SHIRIKA LINAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA LITATEKELEZA MIRADI MIPYA IPATAYO MITATU KAMA INAVYOAINISHWA HAPA CHINI KUANZIA SEPTEMBA 2022 MPAKA MWAKA 2023

1. UCRT KWA UFADHILI WA PAWANKA FUND OF RSF SOCIAL FINANCELITATEKELEZA MRADI WA " HIV PREVENTION IMPLEMENTATION AND REPRODUCTIVE HEALTH EDUCATION FOR THE WELL BEING OF MAASAI COMMUNITIES" KATIKA WILAYA YA NGORONGOROUTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI ZA KITANZANIA 34,710,000
2. UCRT KWA UFADHILI WA INTERNATIONAL WORK GROUP FOR INDIGENOUS AFFAIRS (IWGIA)ITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA ¨SECURING PASTORALIST LAND THROUGH COMMUNAL CERTIFICATES OF CUSTOMARY RIGHTS OF OCCUPANCY ¨ KATIKA WILAYA YA LONGIDO UTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI ZA KITANZANIA 228,758,166
3. UCRT KWA UFADHILI KUTOKA OPEN SOCIETY FOUNDATIONS ITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA ¨GENERAL SUPPORT" UTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI 115,700,000

MIRADI HII YOTE ITATEKELEZWA KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI HUSIKA PAMOJA NA VIJIJI.

KWA MAWASILIANO ZAIDI director@ujamaa-crt.or.tzna manager@ujamaa-crt.or.tz.

217045102




Mfanyakazi katika mradi wa ujenzi wa Blue Amber, Zziadi Haji akizungumza na waandishi wa habari kuhusu madhara waliyopata baada ya serikali kusitisha mkataba wa ukodishwaji wa ardhi kwa Kampuni ya Pennyroyal Limited na kusababisha wafanyakazi 150 kuathirika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zaidi ya wafanyakazi 150 wapoteza kazi kusitishwa mradi ujenzi wa hoteli

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAFANYAKAZI 150 wa Mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota tano Blue Amber, wamepoteza kazi baada ya Wizara ya Ardhi kusitisha mkataba wa ukodishaji ardhi kwa Kampuni ya Pennyroyal Zanzibar licha ya kuwapo amri ya Mahakama ya kutaka ujenzi kuendelea.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wafanyakazi hao wamesema wamepokea kwa mshtuko mkubwa taarifa za kusitisha ujenzi wa hoteli hiyo na nyumba za makazi baada ya mfumo wao wa maisha kuvurugika pamoja na familia zao.

"Tumepokea kwa mshtuko mkubwa sana kusitishwa kwa ujenzi wa mradi sasa hatuna kazi ya kufanya hali ya maisha imekuwa ngumu," alilalamika dereva Ziada Haji Makame.

Fundi mashine, Haji Zaja Haji, alisema mradi wa ujenzi wa hoteli hiyo ya kimataifa ulikuwa umefikia hatua kubwa na tangu ulipoanza vijana wengi wamenufaika katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

"Tunaomba serikali kuangalia upya madhara ya kusitisha mkataba wa ukodishwaji wa ardhi kwa maendeleo ya sekta ya uwekezaji vitenga uchumi Zanzibar," alisema Haji Ali Haji.

Kwa upande wake, John Haji Khamis, alisema kitendo cha kusitisha mkataba wa ukodishwaji wa ardhi kunaweza kurudisha nyuma wawekezaji ambao wameanza kujitokeza kuanzisha miradi katika sekta ya uwekezaji Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo habari na mmiliki Kampuni ya Pennyroyal, Brian Thomson, "usitishaji wa mkataba wa ukodishwaji wa ardhi umetolewa licha ya Kampuni ya Pennyroyal ilikuwa imepokea amri kutoka Mahakama Kuu ya kuendelea na ujenzi."

Akifafanua katika taarifa hiyo alisema, mwaka 2014 kampuni yake ilipata hatimiliki hekta 411 baada ya kukamilisha usanifu wa mradi, ukawasilishwa na kuidhinishwa na Mamlaka ya Kukuza Uchumi Zanzibar (ZIPA) na kupewa hadhi ya mwekezaji wa kimkakati Zanzibar.

"Uidhinishaji mwingine wote wa kisheria ikiwamo cheti cha tathimini ya athari kwa mazingira ulitolewa na mamlaka zote husika.

Alisema Kampuni ya Pennyroyal imeanzishwa mwaka 2012 na kupewa hati miliki mwaka 2014 pamoja na kibali cha uwekezaji mwaka 2018 baada ya kukamilisha sifa na masharti ya uwekezaji vitenga uchumi Zanzibar.

Hata hivyo, Brian katika taarifa hiyo alisema Juni mwaka 2021, Kampuni ya Pennyroyal Limited iliarifiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuwa serikali ilikusudia kutoa sehemu ya ardhi chini ya umiliki wake kwa mwekezaji kutoka nchini Dubai (UAE).

"Hii ilifuatiwa na barua kutoka kwa serikali kwamba ilikuwa ikitaka kutekeleza agizo la Mahakama Kuu ambapo kampuni ya wahusika wengine ilishinda kesi ilihusisha viwanja namba 1107 na 1113, viwanja hivyo vikiwa katika sehemu ya ardhi ya Pennyroyal.

"Tumejitahidi kuhakikisha mradi huu hauporomoki hata hivyo jitihada zetu zimeambulia patupu kwani serikali imekataa kubadili msimamo wake tumewajulisha wamiliki wote watarajiwa wa nyumba ambazo walikuwa wamewekeza katika aina tofauti kuhusu yaliyojitokeza," alisema Brian katika taarifa hiyo.

"Viwanja vinavyodaiwa na serikali kuwa na mgogoro ni hekta 20 kati ya hekta 411 zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni ya Pennyroyal Limited tangu kuwekeza mradi huo.

Hatua ya serikali kusitisha mkataba wa ukodishwaji wa ardhi kwa Kampuni ya Pennyroyal imeibua mjadala mkubwa kutokana na kujitokeza wakati serikali ikiendelea na utekelezaji wa mpango wa kukuza uchumi kupitia mpango wa uchumi wa buluu.

Kwa upande wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudriki Ramadhan Soraga, alisema serikali imesitisha mkataba wa ukodishaji wa ardhi lakini Kampuni ya Pennyroyal wanaendelea kumiliki kibali cha uwekezaji.

"Mkataba wa ukodishwaji wa ardhi kweli umesitishwa, lakini bado wanaendelea kumiliki kibali cha uwekezaji wakati kesi inaendelea mahakamani na kwa upande wa serikali suala hili lipo kwa mwanasheria mkuu wa serikali," alisema Waziri Soraga.

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua mama mkwe wake

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu mkazi wa Kaliua Mkoa wa Tabora, Gibe Masasila (40) kunyongwa mpaka kufa kwa kosa la kumuua mama mkwe wake Kabura Manyakenda.

Masasila alimuua mkwewe huyo kwa kumcharanga mapanga kichwani, shingoni na mkononi na kufariki dunia papo hapo.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Geita mwenye mamlaka ya ziada, Cleofas Waane, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Mkazi Mfawidhi Waane alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali Winfrida Ernest, ulipeleka mahakamani mashahidi sita na vielelezo vitatu ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alimuua mama mkwe wake kwa kukusudia.

Pia alisema upande wa utetezi uliokuwa ukiongozwa na Wakili wa Kujitegemea Nestory Kuyula, haukuwa na shahidi yeyote zaidi ya mshtakiwa kujitetea peke yake.

Hakimu Waane alisema mshtakiwa alikuwa amemwoa Christina na walikuwa wakiisha Kaliua mkoani Tabora na Februari 15, 2018 mshtakiwa pamoja na mtu mmoja aitwaye Mateso walikwenda senta ya Kijiji cha Bwenda wilayani Bukombe kunywa pombe na ilipofika majira ya saa 2:00 usiku, walikwenda nyumbani kwao na mke wake aitwaye Christina.

Alisema walipofika, walimkuta mama mkwe wake Kabura Manyakenda akiwa anamuosha mjukuu wake na mkamwana wake aitwaye Pili Robert aliwapatia viti na wakakaa nje ya nyumba wakawa wanaota moto.

Hakimu alisema baada ya shahidi wa Jamhuri Pili Robert kuingia ndani ya nyumba hiyo, mtu mmoja aitwaye Mateso alimfungia Pili mlango kwa nje ndipo mshtakiwa Masasila alichukua panga na kuanza kumkatakata mama mkwe kichwani, shingoni na mkononi na kufariki dunia papo hapo.

Waane alisema wakati mshtakiwa akimkatakata mapanga mama mkwe wake, shahidi Pili Robert alikuwa akimwona kwa kuchungulia kwenye dirisha ya nyumba hiyo kwa sababu ya mwanga kwa kuwa kulikuwa na moto nje pamoja na taa za Sola.

Alisema baada ya mshtakiwa huyo kusikia kelele kutoka kwa Pili Robert akiwa ndani ya nyumba na kuona mama mkwe wake kafariki dunia, alikimbia na kutokomea kusikojulikana.

Baada ya kitendo hicho, majirani walifika eneo la tukio na kumfungulia mlango Pili Robert na polisi pia walipofika ndipo Pili Robert aliwaambia kuwa mtu ambaye amemuua mama ni mume wa Christina anayeitwa Gibe Masasila. Alisema polisi baada ya kupewa taarifa hizo, walimchukua mke wa mshtakiwa ambaye aliwapeleka polisi nyumbani kwa mshtakiwa Kaliua mkoani Tabora na kumkamata mshtakiwa huyo na kumfikisha kituo cha polisi Bukombe. Baada ya kufikishwa kituoni, mshtakiwa alihojiwa alikiri kumuua mama mkwe wake kwa sababu alimkataza mtoto wake Christina kuolewa na Masasila.

Hakimu Waane alisema chanzo cha kifo cha marehemu baada ya kufanyiwa uchunguzi, daktari alibaini kuwa ni kuvuja damu nyingi baada ya kupata majeraha makubwa sehemu za kichwani, shingoni na mkononi.

Waane alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote, hivyo kumtia hatiani mshtakiwa kwa kosa la kumuua mama mkwe wake kwa kukusudia.

Kabla ya kutolewa hukumu, Hakimu alimtaka mshtakiwa ajitetee ili kumpunguzia adhabu ndipo wakili wake Kuyula akaomba mahakama impunguzie adhabu mteja wake kwa madai kuwa amekaa muda mrefu gerezani pia ana familia inamtegemea.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Ernest, ulidai kuwa hauna kumbukumbu za makosa ya nyuma ya mshtakiwa bali aiombe mahakama itowe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Waane alitupilia mbali utetezi huo na kusema adhabu ya kesi ya mauaji ya kukusudia ni moja tu, hivyo mahakama inamhukumu mshtakiwa kunyongwa mpaka kufa na kama kuna upande ambao haujaridhika na hukumu hiyo, rufani iko wazi.

## Daktari aeleza alivyogundua damu tumboni

Na Grace Gurisha

DAKTARI Bingwa wa Uchunguzi wa Maiti, Emaeli Mushi (64), kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili ameieleza Mahakama kwamba wakati anafanya uchunguzi wa mwili wa Novatus Busanya alikuta zaidi ya lita tatu za damu katika mfuko unaohifadhi vitu vya ndani ya tumbo.

Pia amedai alibaini damu hiyo imetokana na Busanya kupata majeraha mengi ya risasi, ambapo risasi ilirarua ini, tumbo la chakula na utumbo mdogo na watu wanaodaiwa ni majambazi.

Dk. Mushi alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Joyce Minde wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakati akitoa ushahidi wake katika kesi ya mauaji inayowakabili Idd Mussa, Said Adam na Lutofyo Hans ambao wanashtakiwa kumuua Busanya.

Alidai Agosti 17, 2015 alikuwa zamu katika hospitali hiyo saa 5:00 asubuhi na alipigiwa simu na Mkuu wa Kitengo cha Mochwari kuwa kuna mwili anatakiwa akaufanyie uchunguzi.

"Nilikwenda hadi kwenye chumba hicho na kulikuwa na askari mmoja na ndugu wawili kwa ajili ya utambuzi wa mwili, mwili ulitambuliwa na mkuu wa kitengo hiki alinipa fomu ambayo inaniamuru nichunguze maiti.

"Nilianza uchunguzi nikiwa na msaidizi wangu mmoja. Niliangalia nje na ndani ya mwili, niliona mtiririko wa damu na kidonda mithili ya kidonda cha risasi eneo la chembe ya moyo,"alidai Dk. Mushi

Pia alidai kwamba baada ya kuangalia mwili na majeraha hayo alibaini Busanya alifariki dunia baada ya kububujikwa na damu nyingi hali iliyosababisha kuishiwa damu kabisa. Baada ya hapo, alidai kuwa aliacha marehemu anaandaliwa akaenda kuandaa ripoti.

Dk. Mushi aliomba mahakama hiyo kupokea ripoti ya uchunguzi kama kielelezo katika kesi hiyo na Mahakama ikakipokea kielelezo hicho.

Alidai kuwa anafanya kazi katika hospitali hiyo, idara ambayo inahusika na kuchunguza mwenendo wa magonjwa ya binadamu na uchunguzi wa maiti za binadamu.

Akijibu maswali ya Wakili wa mshitakiwa huyo, Godfrey Kizito, Dk Mushi alidai kwamba si wajibu wake kukumbuka mashahidi waliotambua mwili wa marehemu kama walikuwa wa kike au wa kiume.

"Ni karibu miaka saba sasa na kila siku nafanya uchunguzi wa miili mitatu. Kwa hiyo si rahisi kuwakumbuka mashahidi wawili na pia si jukumu langu kukumbuka tarehe kwa sababu kila kitu nimejaza kwenye fomu ya uchunguzi," alidai.

Pia alidai kwamba risasi hiyo haikutokeza nyuma ya mwili wa marehemu kuhusu suala la kuiona risasi alidai si rahisi sana kuiona kutokana na damu nyingi kuganda kwenye tumbo hilo.

Inadaiwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo Agosti 17, 2015 maeneo ya Changanyikeni ndani ya wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam kwa kumuua Novatus Busanya.

# Mwinyi amhakikishia IGP Wambura ushirikiano

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema serikali itatoa kila aina ya msaada kuhakikisha Jeshi la Polisi linatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Dk. Mwinyi alisema hayo Ikulu Zanzibar, alipozungumza na Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania (IGP) Camillus Wambura.

Alisema serikali inatambua uwapo wa changamoto mbalimbali zinazolikabili jeshi hilo na kubainisha azma ya serikali katika kuzitafutia ufumbuzi ili kuliwezesha jeshi hilo kutekeleza vyema majukumu yake.

Alisema lengo la kuwapo vyombo vya ulinzi na usalama likiwamo Jeshi la Polisi ni kuhakikisha kunakuwapo usalama wa kutosha nchini, huku akibainisha ushirikiano kuwa ndio kichocheo cha kuleta ufanisi wa vyombo hivyo.

Rais Dk. Mwinyi alieleza kuwa serikali inaridhishwa na utendaji kazi wa jeshi hilo na kusisitiza azma ya kuendeleza ushirikiano mkubwa uliopo kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na jeshi hilo.

Dk. Mwinyi alimpongeza IGP Wambura kwa uteuzi aliopata katika chombo hicho kikubwa na chenye umuhimu mkubwa katika usalama wa nchi.

Naye IGP Wambura, alisema Serikali ya Tanzania, imekuwa katika juhudi kubwa ya kuipatia ufumbuzi changamoto ya upungufu wa vifaa na vitendea kazi muhimu vya jeshi hilo, husuan katika nyanja ya usafiri.

Alisema pamoja na serikali kutoa fedha za kutosha kwa jeshi hilo kwa jili ya ununuzi wa vifaa, hivi karibuni imepokea msaada mkubwa wa magari 72, huku mengine 78 yakiwa njiani kuja nchini.

"Kuna magari mengine 117 yanaendelea na matengenezo kiwandani kwa ajili ya jeshi letu na mara tu yatakapokamilika yataletwa hapa nchini," alisema.

IGP Wambura alisema ugavi wa magari hayo tayari umefanyika na Jeshi la Polisi Zanzibar limepatiwa magari 10 kwa ajili ya mikoa mitano, Chuo cha Polisi Ziwani pamoja na Kikosi cha Kutuliza Ghasia 'Field Force Unit'.

Aidha, alisema mikoa hiyo pamoja na mingine ya Tanzania Bara itaendelea kupatiwa magari hayo kadri yatakavyowasili nchini.

Kuhusu kukosekana kwa usalama katika mipaka ya Zanzibar, IGP Wambura alisema, kwa kuitikia agizo za Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu, jeshi hilo linalifanyika kikamilifu suala hilo kwa kuzingatia umuhimu wa usalama nchini.

Alisema kwa kuanzia wamefanya kikao muhimu kilichowashirikisha maofisa wa jeshi hilo kutoka pande mbili za Muungano ili kubaini chanzo cha tatizo hilo pamoja na kuzingatia rasilimali watu kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.



Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama la Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Ernest Kimaya (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa maandalizi ya maadhimisho ya Wiki ya Viziwi Duniani kitaifa itakayofanyika Mkoa wa Mtwara mwishoni mwa mwezi huu. Kushoto ni Meneja mradi wa shirikisho hilo, Novatus Rukway na Ofisa Jinsia wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), Lupi Mwaisaka. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Jela miaka 30, viboko 12 wizi mil. 3/-

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kata ya Kilolambwani, Tarafa ya Mchinga, Hamisi Said Kibunda (34), mjini hapo, amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela na kuchapwa viboko 12 baada ya kukutwa na hatia ya wizi wa Shilingi milioni tatu.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya wilaya hiyo, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea ambaye aliiomba Mahakama imwonee huruma kwa kutompa adhabu kali akidai ni kijana anayehitajika kutumika kujenga uchumi wa taifa lake.

Pia alidai ana familia inayomtegemea akiwamo mke, mtoto na wazazi ambao ni wazee na kama akipewa adhabu hiyo watakosa huduma zake.

Hata hivyo, utetezi wake haukumsaidia baada ya Mwanasheria wa Serikali, Rabia Ramadhani, kuiomba Mahakama kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia ya aina hiyo.

Rabia alidai kitendo cha kutumia silaha husababisha mazingira ya hatari na hasara kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja na taifa.

Hakimu Batraine akitoa hukumu alisema, amesikiliza utetezi wa pande zote mbili, lakini kutokana na uzito wa kosa anamhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani.

Pia Mahakama hiyo, imempa mshtakiwa adhabu ya kuchapwa viboko 12 kwenye makalio.

Ilidaiwa mahakamani hapo na Mwanasheria wa Serikali, kwamba Novemba 2, 2021, katika Kijiji cha Kilolambwani, Wilaya na Mkoa wa Lindi, mshtakiwa akiwa na silaha alivunja duka la Saidi Ramadhani na kuiba fedha taslimu Sh. 3,000,000 na kutokomea nazo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanawake wachangamkie fursa za miradi ya serikali

**SERIKALI** imekuwa ikifanya kila njia katika kuwaendeleza wanawake ikiwamo kuteuliwa katika nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali zikiwamo za kisiasa, utendaji katika utumishi wa umma na taasisi.

Kupitia uteuzi huo, imeshuhudiwa wanawake waking'ara katika kila uteuzi unaofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ikiwamo mawaziri na manaibu wao, makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu, wakuu wa mikoa na wilaya, makatibu tawala wa mikoa na wilaya pamoja na wakurugenzi wa halmashauri.

Licha ya nafasi hizo, hivi karibuni ilishuhudiwa Rais Samia akiwateua majaji wengi wanawake katika Mahakama Kuu ya Tanzania jambo ambalo lilipongezwa na wadau mbalimbali wakiwamo wanaharakati wa haki za binadamu. Hatua hiyo ya uteuzi wa wanawake katika nafasi mbalimbali inalenga kufikia usawa wa kijinsia wa asilimia 50 kwa 50 katika ngazi za uamuzi.

Aidha, juzi wakati akifungua mkutano wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) kuhusu Wanawake na Vijana katika Biashara jijini Dar es Salaam, Rais Samia alisema Sheria ya Ununuzi wa Umma imetoa nafasi kwa wanawake kupewa kipaumbele katika miradi ya maendeleo inayofanywa na serikali.

Kupitia miradi hiyo, Rais alisema asilimia 30 ya miradi hiyo itatolewa kwa kampuni zinazomilikiwa na wanawake, lengo kubwa likiwa kuwawezesha wanawake kiuchumi ili kuwa na uwezo katika umiliki wa uchumi.

Sambamba na hilo, pia serikali imeanza kubadilisha baadhi ya sheria kandamizi zikiwamo zile zinazowanyima fursa wanawake kufanya shughuli kwa amani pamoja na kuondoa vikwazo vinavyowakabili, vikiwamo unyanyasaji wa kijinsia katika biashara.

Pia serikali, katika kuhakikisha azma hiyo inatimia, imezitaka taasisi za kifedha zikiwamo benki kuanzisha madirisha maalum kwa ajili ya mikopo kwa wanawake itakayotolewa kwa riba na masharti nafuu ili kuwaongezea ukwasi na kutimiza ndoto zao za kimaendeleo hasa katika utekelezaji wa miradi ambayo wanapata kazi.

Kwa ujumla, hatua hiyo ya kuwawezesha wanawake ni nzuri na inastahili kuungwa mkono kwa kuwa wanawake ni moja ya makundi ambayo yamekuwa nyuma kimaendeleo kwa muda mrefu kutokana na mfumo dume uliokuwa umeshamiri kwa miaka mingi. Ni imani kwamba wanawake wanapowezeshwa kiuchumi, watatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi kuanzia ngazi ya jamii hadi taifa.

Kutokana na mipango hiyo, ni wakati sasa kwa wanawake kuamka na kuchangamkia fursa hizo za kimaendeleo ikiwamo kuungana na kuanzisha shughuli za kibiashara kwa wale ambao hawajaanza. Kwa wale ambao wameshaanza kupitia vyama na mashirikisho yao, wanapaswa nao kuhakikisha fursa hizo haziwapiti.

Kama alivyosema Rais Samia, kuna miradi mingi kama vile ujenzi wa barabara vijijini na usambazaji wa maji ambapo kampuni za ujenzi na uhandisi zinazomolikiwa na wanawake zinaweza kutekeleza. Wakati ni sasa kwa wanawake kuchangamkia fursa hizo.

Pamoja na hayo, wanawake waonyeshe kuwa wanaweza wanapopewa nafasi hizo kwa kufanya kazi zenye viwango vya kuridhisha na hatimaye kuifanya serikali kuwaongezea zaidi kazi na hatimaye kunufaika kiuchumi na kijamii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Beatrice Moses

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuhuma kujikopesha PSSSF zinawashtua wanachama

**KWENYE** uwanja wa habari zipo taarifa za madai ya kuhojiwa kwa Mkurugenzi wa Ununuzi na Ugavi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma(PSSSF), akihusishwa na matumizi mabaya ya Shilingi milioni 193.

Baraza la Maadili la Taifa ndilo limemhoji kiongozi huyo kutokana na matumizi hayo ambayo kati ya fedha hizo Shilingi milioni 193 amejikopesha milioni 117.88 hatua ambayo inatajwa kuwa ni kinyume cha sera ya mkopo wa PSSSF, huku ikidaiwa kuwa ametumia fedha hizo kununua gari binafsi.

Inaelezwa kuwa alipewa fedha kwa ridhaa ya Kamati ya Mikopo ambayo mkurugenzi huyo ni mjumbe wa kamati hiyo ya sera ya mikopo ya PSSSF ya mwaka 2018 .

Wakili wa Serikali Hassan Mayunga anahoji iweje mkopo huo uidhinishwe na kupitishwa haraka bila kufuata taratibu? Kwa upande wake kiongozi huyo akiongozwa na wakili wake amezikana tuhuma hizo akidai kuwa alifuata utaratibu ili kupata mkopo huo.

Hizo ni taarifa ambazo pengine kutokana na jukumu ambalo PSSSF inahusika nalo kwenye jamii hasa kwa wanachama wake linaongeza mapigo ya moyo. Ni kwa kuwa ni wazi kunazuka maswali mengi ikiwamo ni namna gani fedha zao zipo salama kama mtu mwenye dhamana hiyo anatuhumiwa kuzitumia pengine kwa njia inayohitaji kuhojiwa.

Kuanzishwa kwa PSSSF Oktoba 20, 2017 kunakuja baada ya serikali kupitisha uamuzi wa kuunganisha Mifuko ya Pensheni ya PSPF, LAPF, GEPF na PPF na kuunda mfuko mmoja wa PSSSF kwa ajili ya watumishi wa umma, na sheria inayoanzisha taasisi hiyo kupitishwa na bunge Januari 2018.

Wanachama wa mfuko huu wapo kwenye sekta mbalimbali ni kulingana na utumishi wao, ambapo serikali kwa nia njema iliona ni vyema kuanzishwa kwa mfuko huo ili kuwajengea mazingira ya kuishi kwa utulivu mara baada ya kustaafu ama wanapokumbana na changamoto nyinginezo zinaweza kufuata baada ya maisha ya kazi.

Kuibuka kwa tuhuma kama hizo siyo habari njema maana zinazusha hofu na maswali kadhaa, pengine hata kusababisha manung'uniko miongoni mwa wanachama wastaafu wanaosaka mafao yao kwa muda mrefu na hata wanachama wanaoendelea kuchangia fedha zao.

Lakini pia, inaweza kuyumbisha nia njema ya serikali ya uhifadhi salama wa fedha hizo, hivyo inapaswa ifuatiliwe kwa umakini na ukweli ujulikane ili sheria ifuate mkondo wake.

Lakini, pamoja na utaratibu wa kisera na kisheria wa kuchukua mikopo ni jambo la hekima na busara kuwa na miiko na maelekezo ya kupata mikopo hiyo ambayo wanachama wenye fedha zao hawatajihisi vibaya au kulalamikia kile kinachofanyika kwenye akiba zao.

Ni jambo jema kwa Baraza la Maadili la Taifa kuchukua hatua hiyo kudhibiti na kuhakiki mienendo ya viongozi. Baraza lipo chini ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo inafanya kazi kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kama inavyoelekezwa na Katiba ya Tanzania ya 1977.

Katiba inalipa bunge mamlaka ya kuweka misingi ya maadili ambayo yatafafanua nafasi za madaraka ambazo watu wenye kushika nyadhifa hizo watahusika nayo, aidha itawataka watu wanaoshika nafasi fulani za madaraka kutoa mara kwa mara maelezo rasmi kuhusu mapato, rasilimali na madeni yao.

Pia kipo kipengele cha kupiga marufuku mienendo na tabia inayosababisha kiongozi kuonekana hana uaminifu, anapendelea au si muadilifu au anaelekea kukuza au kuchochea rushwa katika shughuli za umma au anahatarisha maslahi au ustawi wa jamii na kingine kinataka kufafanua adhabu zinazoweza kutolewa kwa kuvunja misingi ya maadili.

Wakati katika kipengele kimojawapo kinabainisha kuwa baraza hilo litaweka masharti mengine yoyote yanayofaa au ambayo ni muhimu kwa madhumuni ya kukuza na kudumisha uaminifu, uwazi, kutopendelea na uadilifu katika shughuli za umma na kwa ajili ya kulinda fedha na mali nyinginezo za Umma.

## Tume ya ardhi yatoa angalizo upangaji vijiji

Na Salome Kitomari

TUME ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, imesema kuwa migogoro ya vijiji, kugawanywa kwa maeneo ya utawala na uelewa duni wa wananchi kuhusu kupanga ardhi, ni tatizo katika kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni jijini Dodoma na Mkurugenzi Mtafiti wa Tume hiyo, Joseph Paul na Ofisa Mipango Miji na Vijiji wa tume hiyo, Mapambano Madebo, wakati akizungumza na waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), kuhusu uhifadhi na mazingira kwa ufadhili wa USAID, Tuhifadhi Mazingira.

Madebo alisema tatizo kubwa ni vijiji vingi kuwa na migogoro mikubwa huku vingie vikiwa na migogoro sugu baina ya mtu na mtu, mwekezaji na kijiji au hifadhi na kijiji.

Alisema jingine ni uelewa mdogo wa wananchi hasa wanapopewa taarifa za umuhimu wa matumizi bora ya ardhi, kwamba maofisa wanapokwenda huonekana kama wameenda kuwapora ardhi jambo linalozua mtafaruku.

"Sera na sheria zinaelekeza miradi kuanzia chini hasa kwenye ardhi ambayo ni kwa wananchi wenyewe na sio kuibuliwa juu, tunaelimisha jamii kuibua umuhimu wa kupanga ardhi yao ambayo itakuwa suluhisho la migogoro ya wanyamapori na binadamu na baina yao," alisema.

Alisema tatizo jingine ni mitazamo tofauti ya kisiasa miongoni mwa wananchi kutokana na itikadi zao, na kwamba wengine huunga mkono au kukataa kulingana na anayeongoza kijiji husika au vitongoji.

Kwa mujibu wa Madebo, tatizo jingine ni kugawanywa kwa mipaka ya utawala ambao humega vijiji na kuharibu mpango wa matumizi bora ya ardhi uliofanyika kwa gharama.

Mkurugenzi Paul alisema wanatarajia kutoa tuzo kwa halmashauri zilizofanya vizuri kwenye kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi.

"Tunatoa elimu kuhusu umuhimu wa kupanga vijiji kwamba eneo fulani ni la kulisha wanyama, kunywesha, kilimo, huduma za kijamii na nyinginezo muhimu pamoja na uwekezaji. Tunapata shida kwamba jamii haioni umuhimu wake licha ya kwamba uamuzi unatakiwa kuanzia kwao," alisema.

Alisema kuna vijiji vina migogoro kwasababu wananchi wameweka makazi kwenye njia ya kupita wanyama (shoroba) na maeneo ya mtawanyiko, na kwamba ili kupima kijiji kimoja ni wastani wa Sh. milioni 12 hadi 15 kutegemea na ukubwa wake.

Naye, Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji wa Malisho na Raslimali za Vyakula vya Mifugo, Asimwe Rwiguza, alisema maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho kwenye vijiji mbalimbali nchini ni hekta milioni 3.180.

# Bil. 1/- kukuza uandishi soko la ubunifu

Na Jenifer Gilla

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema serikali imetenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya kukuza soko la vitabu vya uandishi ubunifu wazawa.

Mkenda aliyasema hayo juzi katika hafla ya uzinduzi wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu iliyofanyika katika ukumbi wa Benki ya CRDB, Dar es Salaam kwa lengo la kuwanufaisha watunzi, wachapaji, wachapishaji na wasambazaji wa kazi hiyo nchini.

Alisema utekelezaji huo unatokana na mapendekezo ya wadau wa fani waliokutana na serikali Machi 9, mwaka huu, ambao pamoja na mambo mengine walisema uchapaji, uchapishaji na usambazaji wa vitabu unapitia changamoto nyingi zinazoyumbisha uendelevu wa fani hiyo.

Pia Waziri Mkenda alisema fungu hilo litatumika kununua kazi ya uandishi bunifu iliyoshinda tuzo, ili kufidia gharama za uchapishaji na kuzisambaza maeneo mbalimbali ikiwamo shuleni na kwenye makataba za taifa kurahisisha soko na kuhakikisha zinasomwa kwa wingi na jamii.

"Ninatumaini kwamba huu ni mwanzo mzuri wa kuhakikisha tunachochea uandishi bunifu na usomaji wa vitabu ambao ni janga la dunia na ni kubwa zaidi Tanzania, usomaji wa vitabu umepungua sana. Kunapokuwa na mitandao ya kijamii hali inakuwa mbaya zaidi," alisema.

Aidha, Mkenda alisema katika tuzo hizo mshindi wa kwanza atazawadiwa Sh. milioni 10, wa pili Sh.milioni saba huku mshindi wa tatu akipata Sh.milioni tano.

Kwa mujibu wa Mkenda, bajeti ya mwaka ujao wanategemea kutenga fedha kwa ajili ya kununua vitabu vya ithibati vya kutosha na kuvisambaza shuleni, ili watoto waweze kuvipata kwa urahisi na kuchochea fani ya uandishi bunifu.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Francis Michael, Kamishna wa Elimu nchini, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema wizara hiyo inaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na sekta binafsi ili kuimarisha utoaji wa elimu bora nchini.

Pia alisema itahakikisha tuzo hiyo inatolewa kila mwaka ili kuifanya fani hiyo iwe katika viwango vinavyotarajiwa na kunufaisha vizazi vijavyo.

Aidha, kamishna huyo aliwaomba waandishi hao kutumia kalamu zao kuandika hadithi za kumpigania mtoto wa Tanzania na kumlinda dhidi ya vitendo vya unyanyasaji vilivyoshamiri katika jamii kwa kuwa mtoto ni rasilimali muhimu katika jamii.

"Kikosi hiki cha jeshi la kutumia kalamu kimpiganie mtoto wa Tanzania, mkisoma magazeti ya leo mtatokwa machozi, watoto waliolawitiwa. Nomba enyi waandishi wabunifu wa vitabu nendeni mkapiganie watoto. Kwa kufanya hivyo nchi yetu itajenga watoto imara wenye tabia na mitazamo imara," alisema Mtahabwa.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo hiyo, Prof. Penina Mlama, alisema dirisha la upokeaji wa miswada ya uandishi bunifu limefunguliwa jana hadi Novemba 30, mwaka huu, na kwamba zitahusisha uandishi wa riwaya na ushairi.

Prof. Mlama ambaye ni mwandishi bunifu mkongwe alisema mchakato wa kutafuta washindi utaanza Desemba, 2022 hadi Machi 2023, na washindi watatangazwa kila Aprili 13, mwaka 2023, siku ya kumbukumbu ya kuzaliwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Mlama alisema fani hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa lunga ya Kiswahili ambacho sasa kinapaa kimataifa kutokana na kazi hizo kutumika sehemu mbalimbali ikiwamo kufundishia lugha hiyo shuleni.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (wa pili kulia) na Kaimu Mkurugenzi Mkazi Benki ya Dunia, Preeti Arora (kushoto), wakizindua Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi wenye lengo la kuleta mageuzi ya utoaji wa elimu ya juu (HEET), jijini Dar es Salaam jana. Vyuo 14 vitanufaika kupitia mradi huo. Kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Dk. Francis Michael. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali kuendelea kuijengea uwezo TMA

Na Faustine Feliciane

SERIKALI imesema itaendelea kuijengea uwezo Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ili kuendelea kutoa huduma za viwango vya juu kwenye taarifa za utabiri.

Akizungumza Dar es Salaam jana kwa niaba ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliyekuwa mgeni rasmi kwenye kongamano la 15 la kimataifa la watumiaji wa huduma za satellite za kampuni ya EUMETSAT kutoka nchi za Afrika, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi), Atupele Mwakibete, alisema serikali inatambua umuhimu wa taarifa za hali ya hewa kwa maendeleo endelevu ndiyo maana inajitahidi kuijengea uwezo TMA ili kuifanya kuendelea kutoa taarifa sahihi za utabiri. "Utabiri wa uhakika na wa muda sahihi ni kiini cha maendeleo kwa jamii na Serikali, kwa kulitambua hili Wizara imeendelea kuijengea uwezo Mamlaka kwa kufanikisha mipango mbalimbali," alisema Mwakibete.

Aidha alisema tayari serikali imenunua rada saba za hali ya hewa ambazo zitafungwa kwenye mikoa mbalimbali kuiwezesha TMA kufuatilia mienendo ya hali ya hewa.

"Rada hizi tayari baadhi zimeshafungwa, zingine ziko kwenye hatua ya kukamilishwa kutengenezwa kabla hazijaja kufungwa, kuna rada zitafungwa pembezoni mwa nchi, mikoa kama Mtwara ambayo itamulika mpaka nchi jirani ya Msumbiji. Iko ambayo itafungwa Kigoma lakini iko nyingine pale Mwanza ambayo hii ina uwezo wa kumulika mpaka makao makuu ya nchi, Dodoma," alisema.

Naibu Waziri aliipongeza kampuni ya EUMETSAT kwa uamuzi wa kuja na aina mpya satellite wanayotarajia kuirusha angani Desemba, mwaka huu.

"Nimeambiwa satellite hii mpya watakayoirusha ni ya kizazi cha tatu ukiondoa hii tunayoitumia sasa hivi ya kizazi cha pili. Satellite hii mpya itakuwa na uwezo mkubwa zaidi, hivyo itatusaidia Tanzania katika kupata picha kamili na taarifa sahihi za hali ya hewa," alisema Mwakibete.

Akizungumza juu ya satellite hiyo mpya, Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk Agnes Kijazi, alisema kampuni hiyo ya EUMETSAT imekuja na kizazi hicho cha tatu cha satellite yake ambayo itakuwa na uwezo mkubwa zaidi.

"Satellite hii waliyoizindua ina uwezo wa kupiga picha eneo kubwa zaidi na kwa muda mfupi. Hii itaondoa changamoto ya sasa ya uhakika wa picha zinazopigwa mfano kwenye mawingu, itafanya wataalamu kuelewa kirahisi ukubwa wa mawingu ambapo itawezesha sasa kutoa utabiri wa uhakika zaidi," alisema Dk. Kijazi.

Pia alisema kongamano hilo la 15 linalofanyika Dar es Salaam kwa siku nne, limehusisha watumiaji wa satellite za kampuni hiyo kutoka nchi 54 za Afrika.

Nchi hizo zimewakilishwa na wakurugenzi wa Mamlaka za Hali ya Hewa huku lengo la kongamano hilo ikiwa ni kuangalia taarifa za satellite na changamoto zake.

Alisema kuwa satellite mpya itakayorushwa Desemba, mwaka huu, itaanza kutoa taarifa zake kwa nchi za Afrika baadaye mwakani.

Kongamo hilo pia limehusisha wawakilishi kutoka Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Ulaya (SADC).

# DC Gondwe ataka waharibifu wa miundombinu maji wakamatwe

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, amewataka wananchi kulinda miundombinu ya maji kwa hali na mali na kuwafichua watu wanaojaribu kuihujumu ili wakamatwe.

Alitoa wito huo jana wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa Mkoa wa Dar es Salaam, ilipotembelea mradi wa maji Makongo hadi Bagamoyo unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia (WB).

Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama hivyo wanapaswa kuwa walinzi wa miundombinu hiyo ambayo ndiyo inasambaza maji kwao.

Serikali, alisema inatumia gharama kubwa sana kujenga miundombinu hiyo hivyo wote watakaobainika kujaribu kuihujumu watachukuliwa hatua kali.

Alisema serikali inatoa huduma ya maji kwa gharama nafuu kuliko ilivyo kwa watu binafsi, ambapo gharama ya ndoo moja ya maji ya DAWASA inauzwa kwa Sh. 33 tofauti na bei za mtaani.

"Hivyo kwa wanaohujumu miundombinu ya maji wanaharibu upatikanaji wa huduma kwa wananchi wengine na kuleta hasara kwa serikali na kwao wenyewe mkiwaona toeni taarifa kwa mamlaka husika," alisema.

Naye Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Adam Ngalawa, alisema wananchi wanapaswa kuitunza miundombinu ya maji ili iweze kutoa huduma ya maji iliyokusudiwa na kwa uhakika.

"Kamati inapenda kuwatoa wasiwasi wananchi wa maeneo ya Mbweni, Tegeta A, Goba, Madale na Makongo ambao bado hawajapata maji, kuwa kamati imetembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa maji Makongo hadi Bagamoyo na kuridhika na kasi ya utekelezaji," alisema.

Ngalawa alisema ujenzi wa matangi ya maji ya Vikawe, Mbweni na Tegeta A, ambayo yote yamekamilika kwa asilimia kubwa, hivyo wawe wavumilivu na wawe na matumaini makubwa ya upatikanaji wa maji ndani ya mwaka huu.

"Kamati inapenda kumpongeza sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwekeza kiasi cha bilioni 65.4 kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma," alisema.

Ngalawa aliitaka DAWASA kukamilisha utekelezaji wa mradi kwa wakati ili ifikapo Desemba wakazi wapate huduma.

Mkurugenzi wa Miradi wa DAWASA, Mhandisi Ramadhani Mtindas, alisema utekelezaji wa mradi umehusisha ujenzi wa matenki matatu makubwa ya ujazo wa lita 5,000,000 kila moja.

Alisema mradi pia umehusisha ujenzi wa vituo viwili vya kusukuma maji, ulazaji wa bomba kubwa kwa umbali wa kilomita 1,200 pamoja na mabomba ya ukubwa kuanzia inchi 16, 14, 12, 10, 8, 6, 4 na inchi 2 kwenda kwa wateja.

Alifafanua kuwa mradi umefikia asilimia 87, ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba mwaka huu, hivyo wananchi wawe na subira wakati Mamlaka inakamilisha kazi hii.



Mkurugenzi wa Miradi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Ramadhani Mtindasi (kulia), akitoa maelezo kwa viongozi wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Dar es Salaam, kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji wa Makongo hadi Bagamoyo, wakati wa ziara yao ya siku moja kukagua miradi hiyo mkoani humo jana. Wa tatu kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wakazi Kihanju kunufaika mradi kisima majisafi

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti na Water Aid Tanzania wamezindua mradi wa kisima cha maji chenye thamani ya Sh. milioni 293 katika Kijiji cha Kihanju, Kata ya Tambukareli, Wilaya ya Itigi, mkoani Singida katika juhudi za kuwapelekea majisafi na salama.

Mradi huo una uwezo wa kuhudumia watu zaidi ya 2,000 na ufadhili umefanyika kwa ushirikiano kati ya SBL na Water Aid kwa kujenga kisima na mfumo wake, pampu, tangi la maji na mtandao wa usambazaji maji.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema mradi huo upo chini ya programu yao ya Water for Life na juhudi za ujenzi wa visima vya majisafi na salama umefanyika katika mikoa ya Mara, Iringa, Kilimanjaro, Mwanza, Tanga, Manyara, Ruvuma, Dar es Salaam, Pwani na Dodoma.

Ocitti, alisema mradi huo utalinda afya za wakazi wa Itigi na kuwa chachu ya maendeleo yao ya kiuchumi hasa kwa wanawake ambao hawatalazimika kusafiri tena umbali mrefu na kwa masaa mengi kutafuta huduma ya majisafi.

"SBL ina dhamira ya kisera kuleta ustawi wa jamii yetu, na tumechagua majisafi na salama kama moja ya maeneo manne ya kipaumbele ambayo kampuni yetu imeainisha katika lengo lake la kutoa msaada kwa kijamii tunayoihudumia," alisema Mark.

Alielezea maeneo mengine ambayo SBL imekuwa na mafanikio makubwa, kama utoaji wa ufadhili wa masomo ya kilimo kupitia kilimo viwanda ambao umefadhili wanafunzi zaidi ya 200 tangu 2019, na kampeni ya unywaji kistaarabu ambayo imeelimisha maelfu ya madereva.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliishukuru SBL kwa kutoa msaada huo na kuwa SBL imekuwa mstari wa mbele katika kukuza miradi ya maendeleo nchini inayojenga jamii yenye afya na tija.

"Mradi huo utaongeza juhudi za serikali chini ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP 2025, unaolenga kuhakikisha asilimia 100 ya Watanzania wanapata majisafi na salama na kuboresha huduma za usafi wa mazingira," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Water Aid nchini, Anna Mzinga, alisema shirika lake linajivunia kushirikiana na SBL katika kuhakikisha kuwa maji safi na salama yanapatikana kwa Watanzania hasa wale waishio maeneo ya pembezoni na wasio na uwezo wa kupata mahitaji hayo muhimu.

# Mabadiliko sheria ya ndoa yaja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ameliambia bunge kuwa wiki ijayo Kamati za Bunge za Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na ya Katiba na Sheria zitakutana kujadili marekebisho ya sheria ya ndoa.

Dk. Gwajima aliliambia bunge jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Amina Daud Hassan.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itapeleka bungeni marekebisho ya sheria ya ndoa ili kupunguza changamoto za ndoa za asiri na utotoni.

Akijibu swali hilo, Waziri Gwajima alisema serikali imepokea hoja ya bunge na itawasilishwa kwenye kikao hiko ili kufanyiwa kazi.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kutoa elimu kwa wanawake kuepuka ndoa za siri ambazo zina tatizo la malezi na familia.

Dk. Gwajima akijibu swali hilo, alisema serikali ipo mbioni kukamilisha mwongozo wa taifa wa uendeshaji, usimamizi na uratibu wa mabaraza ya usuluhishiwa wa ndoa na familia.

Alisema mwongozo huo utasaidia kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia taratibu za ufungaji wa ndoa pamoja na kuyajengea uwezo mabaraza ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia ili kuendelea kutoa elimu katika jamii.

Aidha, alisema serikali inatambua kuwa ndoa ni taasisi muhimu katika kuimarisha haki na ustawi wa familia.

"Serikali kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) wa mwaka 2017-18/2021-2022 eneo namba nne inayohusu malezi na mahusiano ya familia imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu malezi chanya na mahusiano ndani ya familia ili kuwa na familia inayozingatia maadili mema," alisema.

Pia katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ritta Kabati, alisema pamoja na suala la ndoa kuna tatizo la malezi kwa watoto kutokana na wazazi kuwapeleka watoto bweni wakiwa wadogo na hivyo kukosa malezi ya wazazi.

Alihoji kwanini serikali isirudishe mitaala ya sayansi kimu ili kusaidia suala la malezi.

Akijibu swali hilo, Gwajima alisema kuna kasi kubwa ya mmomonyoko wa maadili na kusababisha tatizo la ukatili na suala hilo la mitaala wamelipokea watakutana na mamlaka husika.

# TUDARCo yazindua sera za kupinga unyanyasaji chuoni

**Na Waandishi Wetu**

CHUO Kikuu Shirikishi Tumaini (TUDARCo), kimezindua sera mbili za jinsia, lengo likiwa ni kupinga unyanyasaji wa kijinsia kwa wanafunzi katika chuo hicho.

Sera hizo ni ya jinsia, pamoja na ya unyanyasaji ambazo zitawawezesha wanafunzi wa vyuo vikuu kufurahia fursa sawa, haki za binadamu na kutobaguliwa wanapokuwa chuoni hapo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa sera hizo, Mkuu wa TUDARCo, Profesa Burton Mwamila, alisema kupitia sera hizo zitasaidia kuondoa unyanyasaji kwa wanafunzi, licha ya kuwapo kwa kesi nyingi za unyanyasaji chuoni hapo.

Alisema lengo la TUDARco ni kuhakikisha inatokomeza vitendo hivyo na matarajio ya baadaye ni kutokuwapo kwa kesi za unyanyasaji wa kijinsia miongoni mwa wanafunzi na walimu.

"Mimi pia nitawajibika kusimamia sera hizo kwani ni nzuri na zina misingi mizuri. Pia sitaki kusikia TUDARCo kuna unyanyasaji wa kijinsia bali pawe sehemu ambayo hakuna matukio hayo," alisema Prof. Mwamila.

Mratibu wa Kituo cha Usuluhishi na Upatanishi (GEMSAT), Gladness Munuo, alisema sera ya jinsia inaangalia ukuaji wa wanawake vyuoni, mazingira salama kwa wanawake, uelewa kati ya mwanamke na wanaume pamoja na utawala.

Alisema sera hizo zimefanuliwa katika sehemu tisa, kwamba taasisi yoyote ni lazima iwe na kituo cha afya kwa ajili ya wafanyakazi na wanafunzi wa chuo.

"Kila idara lazima iwe na usawa wa wafanyakazi kama ni asilimia 20 kwa 20, kama ni asilimia 10 kwa 10, lengo kuu ni kuondoa unyanyasaji wa kijinsia," alisema Munuo.

Aliipongeza TUDARco kwa kufanikiwa kuishawishi bodi ya chuo hicho kwa kupitisha sera hizo Mei 20, mwaka huu.

Mhadhiri wa TUDARco, Marry Kafyome, alisema: "Tumedhamiria kuzuia vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kwa wana TUDARCo na wadau, pia ni hamu ya chuo kuona kwamba hakuna unyanyasaji kwa watu wote.

"Sera inaonyesha wazi kwamba kwa wale watakaokiuka watachukuliwa hatua za kisheria, maendeleo endelevu yanashirikisha dhana ya watu bila ya ubaguzi uwe la rangi, jinsia au wa kidini," alisema.

***Imeandaliwa na Evence Evarist (DSJ), Victoria Mgodomi, Joram Gervas (TUDARCo)**



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serekumba (wa pili kushoto), akizindua mradi wa kisima cha maji kilichofadhiliwa na Kampuni ya Serengeti Breweries Ltd (SBL) na Water Aid, katika Kijiji cha Kihanjo, wilayani Itigi, mkoani Singida juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mkaazi wa Water Aid, Anna Mzingana (wa tatu kushoto) ni Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vitongoji 37,000 havina huduma ya umeme

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema Wakala wa Nishati Vijijini (REA) unahitaji transfoma 40,000 kusambaza umeme kwenye vitongoji 37,000 ambavyo havijafikiwa na huduma hiyo kati ya vyote 67,000 nchini.

Vilevile, amesema Shirika la Umeme (TANESCO) linahitaji transfoma 50,000 ili kufanya ukarabati kwenye miundombinu yake iliyochakaa.

January aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizundua awamu ya pili ya Kiwanda cha Elsewedy cha kuzalisha transfoma na vifaa vya umeme nchini.

"Uhitaji wa transfoma kwa kipindi cha miaka mitano ni 90,000 na uwezo wa kiwanda hiki ni kuzalisha 2,500 kwa mwaka. Nimeongea na wawekezaji wapanue kiwanda ili kuongeza uzalishaji na wamekubali kwa sababu wana eneo," alisema.

Kuhusu hali ya uhitaji wa umeme nchini, Waziri January alisema umeongezeka kutoka asilimia sita hadi 10 kwa kipindi cha miaka miwili na tayari wameshasambaza umeme vijijini kwa asilimia 80.

Alisema kuna uhitaji mkubwa wa vifaa vya umeme nchini kwa sababu vinaendelea kuharibika licha ya kuwa kuna viwanda vingine sita vya kuunganisha transfoma ambavyo kwa mwaka vinaunganisha transfoma 30,000.

Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Maharage Chande, alisema kuwapo kwa kiwanda hicho kutasaidia kuongeza ajira kwa vijana na Watanzania kunufaika.

Alisema kuzalishwa kwa transfoma hizo nchini kutasaidia kuokoa muda wa mwaka mmoja wa kuagiza nje ya nchi na kupatikana kwa urahisi kwa huduma ya umeme maeneo mbalimbali.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Elsewedy Afrika Mashariki, Ibrahim Qamar, alisema kiwanda hicho kilianza uzalishaji Juni mwaka jana na wanasambaza nyaya za umeme katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

Pia alisema wanasambaza katika nchi za Kenya, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Madagasca na matarajio ni kuanza kuzalisha mita za umeme na vifaa vingine.

Alisema wametoa ajira 15,000 na hadi kukamilisha ujenzi wa kiwanda hicho, watakuwa wamewekeza dola milioni 50.

## RC Mtaka ahadharisha walimu wa kike na 'marioo'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka amesema walimu wa kike ni waathirika wa matukio ya utapeli kutoka kwa vijana wadogo ambao huwalaghai kwa kuwachukulia mikopo.

Akizungumza katika kikao cha uzinduzi wa vitabu vya muongozo wa uteuzi viongozi wa elimu katika mamlaka za serikali za mitaa na mikoa, alisema amekutana na mwalimu aliyechukua mkopo umiza kwa ajili ya kumpa kijana.

Alimtaka Ofisa Elimu kupata muda wa kuongea na walimu hao ambao wanatapeliwa na vijana wadogo kwa kuwachukulia mikopo ya vyombo vya usafiri.

"Vijana hao wakishapata wanaishia mitini huku mwalimu akibaki anahangaika," alisema Mtaka.

"Yanachekesha lakini pia yanaleta shida kwenye utumishi, nimeamua kesi hizi nyingi sana, walimu wa kike huko mtaani kuna mtu anaitwa marioo anaishi kupitia mshahara wako," alitahadharisha.

Wakati huo huo, Mkuu huyo amepiga marufuku kutoa vibali vya uhamisho kwa walimu wa ajira mpya huku akiwataka wafanye kazi katika vituo walivyopangiwa kwa uadilifu.

Alisema wapo walimu ambao wamefanya maombi kwa Mungu kwa muda mrefu ili wapate ajira na hatimaye Mungu akasikia kilio chao na wakapata ajira, lakini siku chache baadaye wanaanza kutoa visingizio ili wahamishwe kituo cha kazi.

Aliwataka kukumbuka ya nyuma kwa kushukuru nafasi ya ajira walizozipata sasa licha ya kuhangaika kwa muda mrefu.

"Wakati unaomba kazi kwenye mfumo hukujua shule unayoenda ulikuwa una muomba Mungu nisaidie nipate ajira hivyo sitarajii mtu mwingine mjinga akamfuata ofisa elimu kumwambia nihamishie kituo fulani," alionya Mtaka.

Alisema mikakati iliyopo ni kuinua kiwango cha elimu kuanzia ngazi za halmashauri, wilaya, mkoa na kitaifa kwa kuondoa sifuri katika shule zote za mkoa wa Njombe.

# Mbunge ashauri mabasi ya shule yaendeshwe madereva wanawake

MBUNGE wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, amesema kuna ongezeko la uhalifu na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye mabasi yanayobeba wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na kushauri magari hao yaendeshwe na madereva wanawake.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mbunge huyo alihoji serikali haioni ni wakati sasa magari hayo kuendeshwa na madereva na makondakta wanawake ili kunusuru hali hiyo.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema "Inawezekana ushauri wake ni moja ya mambo ambayo yataweza kusaidia, tumechukua na zipo hatua nyingine ambazo serikali inachukua tutachukua ili kufanyia kazi ushauri wake matatizo hayo yasijitokeze tena."

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Tauhida Cassian Gallos, alitaka kujua mkakati gani wa kudhibiti ongezeko la uhalifu nchini.

Akijibu swali hilo, Masauni alitaja mikakati mbalimbali ikiwamo kuimarisha doria na kufanya operesheni za kukabiliana na hali hiyo.

Alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi linaendelea na mikakati yake ya kudhibiti vitendo vya uhalifu hapa nchini kwa kuimarisha doria, kufanya misako na operesheni mbalimbali dhidi ya uhalifu na wahalifu.

Pia kutoa elimu kwa jamii kutokujihusisha na vitendo vya uhalifu na kufuata sheria za nchi, kushirikisha jamii kwenye ulinzi wa maeneo yao kupitia dhana ya ulinzi shirikishi.

"Serikali pia imewapeleka wakaguzi wa polisi kwenye kata na shehia ili kushughulikia uhalifu kwa kushirikiana na wananchi," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema kumejitokeza uhalifu unaofanywa na wahalifu wanaojiita panya road na kuhoji serikali ina mikakati gani ya kukukabiliana nalo.

Masauni akijibu swali hilo, alisema serikali inaendelea kukabiliana na uhalifu huo na kwamba Jeshi la Polisi litatoa taarifa namna lilivyoweka mikakati ya kupambana na wahalifu hao ikiwamo Mkoa wa Dar es Salaam.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akimwapisha Tamima Haji Abass, kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania, wakati wa kikao cha kwanza cha mkutano wa nane wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali kujenga miundombinu umwagiliaji hekta 95,000

SERIKALI imesema katika mwaka 2022/23 imepanga kukarabati na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika eneo la hekta 95,000 nchini.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), Charles Mwijage.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua kwanini serikali isishirikishe sekta binafsi katika kilimo cha umwagiliaji ili kutimiza ajenda 10/30.

Akijibu, Mavunde alisema kandarasi 55 zitatolewa kwa sekta binafsi na mpaka sasa mikataba 21 ya makandarasi imesainiwa na serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Alisema serikali katika utekelezaji wa miradi yake mbalimbali sekta ya kilimo imeendelea kushirikiana bega kwa bega na sekta binafsi.

"Kwa muktadha huo, katika miradi ya umwagiliaji ambayo serikali inatekeleza kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kuishirikisha sekta binafsi katika hatua mbalimbali za miradi hiyo ili kufikia malengo ya Agenda 10/30," alisema.

Katika swali la nyongeza, alitaka kufahamu serikali ina mkakati gani wa kutumia mabonde makubwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kuwa mabonde yote yataguswa ukiwamo Mto Ngono.

Mavunde alisema upembuzi yakinifu unafanyika katika mabonde makubwa 22 kwa ajili ya kutumika katika kilimo cha umwagiliaji nchini.

Wakati huo huo, Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi alihoji lini serikali itarejesha utoaji wa ruzuku ya pembejeo za dawa kwa wakulima wa kahawa.

Mavunde akijibu swali hilo, alisema kutokana na kukua kwa teknolojia ambako kumewezesha kugunduliwa kwa miche chotara ya kahawa ambayo ina ukinzani na magonjwa makuu ya kahawa ya kutu ya majani na Chole Buni.

Alisema serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kuzalisha miche bora ya kahawa milioni 20 yenye ukinzani mkubwa wa magonjwa na ambayo hutolewa kwa ruzuku kupitia Taasisi ya Utafiti TaCRI na Bodi ya Kahawa Tanzania.




Habari zote: Augusta Njoji
DODOMA

## Zaidi ya viwanda 130 vinachakata taka ngumu

BUNGE limeelezwa hadi sasa kuna viwanda 137 vya kuchakata taka ngumu nchini.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe alieleza hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Asya Mwadini Mohamed.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji kuna viwanda vingapi vya kuchakata taka ngumu nchini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kigahe alisema viwanda hivyo vimegawanyika katika makundi makuu manne ambayo ni viwanda vinavyotumia taka zitokanazo na chuma (16), viwanda vinavyotumia taka za plastiki (70).

Pia alisema viwanda vidogo vya kutengeneza mkaa mbadala kutoka kwenye mabaki ya kilimo (50), na kiwanda kimoja cha kutengeneza mbolea aina ya mboji inayotokana na mabaki ya vyakula (1).

## Vijana wenye sifa kuwezeshwa fursa ajira nje ya nchi

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imeweka mkakati maalum wa kuhakikisha kuwa vijana wa kitanzania wenye sifa zilizowekwa wanapata fursa za ajira nje ya nchi.

Naibu Waziri, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ng'wasi Kamani.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mkakati gani wa kutumia Balozi za Tanzania kuhakikisha vijana wengi wa kitanzania wanaajiriwa nje ya nchi.

Akijibu swali hilo, Balozi Mbarouk alitaja mikakati hiyo kuwa ni Balozi nje ya nchi zimeendelea kutafuta fursa za ajira kwenye maeneo yao ya uwakilishi na kuingia mikataba ya ajira nje ya nchi inayowawezesha vijana kupata ajira na kuwahakikishia usalama na maslahi yao katika ajira hizo.

"Serikali kupitia Kanzi Data ya Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TAESA), inawawezesha vijana na wataalamu mbalimbali kujiandikisha ili kuwasaidia kuomba nafasi za ajira zinapopatikana nje ya nchi," alisema.

Pia alisema wizara inafuatilia nafasi za ajira zinazotangazwa katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa na kuziwasilisha katika mamlaka mbalimbali ili kusaidia kuwatambua vijana wenye sifa kutoka serikalini na sekta binafsi na kuwashawishi kuomba nafasi hizo.




Ukurasa 12

**Mwiba wa tozo huenda ukaondoka kwenye vidonda**



Ukurasa 13

'Mama' amefariki lakini Mfalme Uingereza akumbushwa haya



Ukurasa 14

**MFALME CHARLES III...**

**Auchukua ufalme bila kujali yaliyopita**


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 14, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


VIPORO MIGOGORO YA VYAMA

# Ofisi ya Msajili yahofiwa pengine haiko huru, wadau wataka katiba kunusuru

**Na Sabato Kasika**

VYAMA vya CUF na NCCR-Mageuzi, vimekumbwa na migogoro ya kiuongozi, ambayo imesababisha baadhi ya wanachama wakiwamo viongozi kufukuzwa na wengine kuzuiliwa kujishughulisha na chochote katika taasisi hizo.

Sintofahamu hiyo ilianzia CUF kutokana na baadhi ya makada wa chama hicho saba akiwamo mgombea mwenza wakati wa uchaguzi mkuu wa 2020, Hamida Abdallah Huweishi, aliyesimama na mgombea urais Profesa Ibrahim Lipumba, kutimuliwa.

Pamoja naye ni kiongozi mwingine Abdul Kambaya, aliyekuwa Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Mahusiano ya Umma. Wote walivuliwa uanachama, kisha wakaenda kushtaki katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, ili kutafuta suluhu.

Mgogoro wa CUF ulianza Novemba mwaka jana baada ya Baraza Kuu la Uongozi Taifa, kutangaza kuwavua uanachama na kutakiwa kukata rufaa ndani ya siku 14 kama watahisi kuonewa.

Hata hivyo, baada ya kutimuliwa walipeleka malalamiko katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa jijini Dodoma, wakidai kufukuzwa kwao ni kukiuka ibara ya 11(6) ya katiba ya CUF inayotaka mtuhumiwa kupewa haki ya kujitetea kabla ya kuadhibiwa kwa kusikilizwa kwanza.

Lakini tangu wapeleke malalamiko yao katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Kambaya kwa niaba ya wenzake anadai hawajapata majibu, huku akidai kuwa ofisi hiyo imekuwa na kigugumizi.

Wakati mgogoro wa CUF ukiwa haujatolewa maamuzi NCCR-Mageuzi nayo imefikisha mgogoro wao katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, hivyo kufanya ofisi hiyo kuwa na viporo vya migogoro ya vyama viwili.



James Mbatia wa NCCR- Mageuzi ambaye mgogoro wa chama hicho, umefikishwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ukiwa umetanguliwa na wa Chama cha CUF. **PICHA: MTANDAO**

### OFISI HAIKO HURU

Kutokana na migogoro kuchukua muda mrefu bila ufumbuzi baadhi ya wadau wanasema pengine kuna mambo yaliyojificha nyuma ya pazia. Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, anasema Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kushindwa kumaliza migogoro ndani ya vyama kwa wakati, huenda haiko huru.

"Kwa mujibu wa Sheria No 5 ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 na marekebisho yake ya mwaka 2019, Ofisi ya Msajili iko chini ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge," anasema Wangwe akifafanua kuwa, waziri huyo ni mwanasiasa anayetokana na chama cha siasa, na kwamba kwa mazingira hayo, hadi yeye ndiye aamue cha kufanya ndipo Msajili wa Vyama vya Siasa atekeleze.

"Ni kwamba, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa haiko huru, hivyo wito wangu ni kwamba sheria hiyo ifanyiwe marekebisho, ili iundwe na watu huru," anasema na anafafanua kuwa, bila kufanya hivyo, migogoro ya vyama inayopelekwa katika ofisi hiyo inaweza kuchukua muda mrefu bila kutatuliwa, na kwamba hali hiyo itaendelea kuzua malalamiko.

"Hivi karibuni, NCCR- Mageuzi walipeleka malalamiko yao katika ofisi ya waziri huyo, kwani Sheria ya Vyama vya Siasa inamtambua kuwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iko chini yake," anasema.

Mdau na mwaharakati wa siasa za kiushindani (jina tunalo) anaungana na Wangwe akisema masuala kama hayo ndiyo yanayoongeza moto wa kuwa na katiba mpya itakayoweka sawa mazingira ya hatma za vyama vya siasa ambavyo havijui wapi pa kukimbilia kwenye mashaka na matatizo hasa migogoro ya kiuongozi.

Anasema wanademokrasia nchini wanatarajia kamati ya kukusanya maoni ya wananchi kuhusu marekebisho ya katiba maarufu 'kikosi kazi' imelipokea suala hilo na kwamba bila kuboresha taasisi hiyo ya kusimamia vyama vya siasa havitakuwa na mazingira bora ya kudumisha demokrasia.

### MWENDO WA KIMYA

Akizungumzia kusuasua Kambaya anadai waliotimuliwa wamehangaika kutafuta haki yao katika ofisi ya msajili kwa muda mrefu, sasa wameamua kukaa kimya ili kuona nini kitatokea baadaye.

"Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inajua ukweli kuhusu mgogoro wa CUF lakini inashindwa kuamua , ndiyo maana imekuwa kimya tangu mwishoni mwa mwaka jana hadi leo," anasema Kambaya.

Kambaya anasema pamoja na ukimya huo, yeye na wenzake wataendelea kusubiri hadi kieleweke, kwa madai kwamba hakutendewa haki, hivyo wataendelea kuitafuta hadi waone hata yao.

"Kukaa kimya ni uungwana, hivyo nasi tumeamua kuwa kimya lakini tukisikilizia kwa karibu kesi yetu kwa Msajili.

**INAENDELEA UK. 14**

# Mwiba wa tozo huenda sasa ukaondoka kwenye vidonda

**Na Nimi Mweta**

SERIKALI imekubali kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu tozo, Wizara ya Fedha, sasa inafanyia kazi maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, chama tawala pamoja na maoni ya wananchi kuhusu kilio hicho cha kukatwa fedha kwenye miamala ya simu na ya kibenki.

Ni maelezo ya karibuni ya Waziri wa Fedha Mwigulu Nchemba, anayesema kuwa nia ya serikali ni kukusanya mapato, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaokwenda sambamba na kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuweka miundombinu wezeshi inayoibua wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa na hatimaye kuinua kipato cha kila Mtanzania.

Kinachoonekana hapo ni kama vile tozo zimeshindikana na sasa ni vyema serikali iangalie mbali zaidi.

Maelekezo yalianzia na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya kuitaka serikali iangalie upya tozo za kupeleka fedha kwa miamala ya simu na kwenye benki.

Hali hiyo ilionekana kuwa ni kielelezo cha kukwama kwa mpango huo uliobuniwa mwaka jana. Si rahisi kusema ni migongano inayoendelea kuhusu tozo hizo, ila inaelekea hatua za kuipanua kutoka kwenye kupeleka fedha kwa simu hadi kutoa fungu la fedha benki ikawa kichocheo cha mzozo na maumivu kwa Watanzania.

Hatua ya kwanza ambayo hazina inatakiwa kuchukua ni kuondoa nyongeza ya tozo katika miamala ya benki na hata ile ya kupeleka fedha kwa simu, ambayo imeanza kutumika. Kwa ujumla katika hali halisi dhana nzima ya tozo imeingia doa na inavyoelekea haikubaliki.

Imekuwa ni kodi kwa fedha unayoipata, wakati ukifanya kazi yoyote na ukilipwa mshahara unakatwa kodi, hivyo ni kama kodi ya kupokea mshahara. Kwa maana hiyo inakuwa kinyume labda hata cha katiba, wakati dhana ya tozo hasa ni kutumia kifaa cha simu na siyo kupokea au kupeleka fedha, kwani hakuna kodi inayoweza kubuniwa kwa jambo hilo. Ni kama kuitoa fedha mfukoni.

Wakati kuna tatizo la ubunifu katika mpangilio wa tozo, lipo jingine pana zaidi la njia ambazo serikali inaweza kutumia kufikia malengo yake ya mapato ili kasi ya maendeleo na kupatikana huduma za jamii iendane na matazamio ya wananchi katika awamu ya sita.

Hatua iliyofikiwa sasa ni kuanza kufilisika kwa ule usemi wa jadi wa 'kutafuta vyanzo vipya vya mapato' kwani hatua zimekuwa zikichukuliwa kuondoa 'kodi nyang'anyi au mbinu nyang'anyi, na sasa hizi tozo zimeingia katika mkumbo huo.

Ni zile mbinu za awamu ya tano ambako Mamlaka ya Kodi (TRA), ililazimisha fedha kutolewa katika akaunti ya kampuni katika benki, ilipe kodi au deni fulani kwa serikali.

Kwa maana hiyo kuna uwanja finyu kwa Hazina kurekebisha tozo bila kuathiri mpango wa matumizi kwa mwaka huu wa fedha, na huedna haitakuwa rahisi pia kwa Waziri Mwigulu, mwenye nia kuweka mkazo wa kutosha katika kubana matumizi ya serikali.

Tayari serikali ilishaelekeza maofisa wakubwa wakiwamo wabunge kukopeshwa magari badala ya kutumia magari ya serikali ila mawaziri wanakuwa na mikopo halafu na magari ya serikali. Ni tozo pia.

Na si ajabu kutumia namba maalum za serikali kunasababisha matumizi makubwa ya fedha kununulia magari, hata kama kwa baadhi yao yatakuwa ni ya mikopo. Ili kupunguza matumizi hayo magari ya serikali yangebaki miongoni mwa wakuu kadhaa wa idara nyeti, na wasaidizi wa karibu huku wale ambao wanafanya kazi kiraia na siyo kijeshi wanunue magari wanayotaka ila wawe na 'fixed allowance' ya kujazia kwani jamii inawahitaji kuwa watembee na kusafiri katika kuwahudumia.

Ila haitakuwa rahisi kwa wakubwa serikalini kufuta utaratibu wa kuhakikishiana 'V8' za kisasa.

Nje ya hatua kama hiyo, siyo rahisi kuona ni wapi serikali inaweza kutafuta kiasi cha fedha kinachokaribiana na Shilingi trilioni moja au kuongeza kodi za hapa na pale, kwani eneo pana la nyongeza kama hiyo ni petroli na dizeli, ambazo sasa kama hazishikiki.

Serikali inaongeza Shilingi bilioni 100 kila mwezi kupunguza makali ya bei ya mafuta, hivyo haina nafasi ya kuongeza bei katika eneo hilo.

Ila ina nafasi ya kuandaa mradi wa haraka wa kubadili matumizi ya petroli na dizeli kwa magari ya serikali kwa kushirikiana na kampuni kubwa za gesi ili vyombo hivyo vitumie gesi ya ndani.

Tatizo kidogo kwa upande huo ni kuwa mkakati huo wa kutumia gesi umekuwa biashara maalum ya Shirika la Taifa la Maendeleo ya Petroli (TPDC) na linatoa zabuni kuanza mradi wa majaribio katika vituo maalum, badala ya kufungulia milango watu wakaanza kubadili injini zihamie gesi.

Kuna karakana kadhaa zinaweza kazi hiyo, na si vigumu kwa wahandisi 'kuteremsha' programu kubadilisha magari na kuanza kuzitumia, yatumie gesi, ila mamlaka elekezi ya EWURA ikishikiriana na taasisi kama Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Shirika Viwango (TBS) wakague magari hayo.

Ukiangalia suala hilo kwa mpangilio endelevu wa matumizi ya fedha serikalini unaona kabisa yako maeneo bayana ya kupunguza matumizi ila itakuwa ni jukumu la Rais Samia Suluhu Hassan kutoa maagizo kwa mfano kwa kuleta 'bajeti ndogo' mwisho wa mwaka, ianze kutekelezwa mwaka mpya ukianza. Kuiachia serikali ifanye kazi hiyo ni kizungumkuti kwani utamaduni wao ni kufurahishana na kujitahidi kuwaaminisha wananchi kuwa wanafanya kazi kubwa sana, wakimtaja mkuu wa nchi kwa sifa ambazo ni pamoja na kusifia kila wakati.




Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba akiwasilisha bajeti ya serikali bungeni ambayo ilihusisha pia muswada wa fedha ulianzisha tozo zinazolalamikiwa. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

> Serikali inaongeza Shilingi bilioni 100 kila mwezi kupunguza makali ya bei ya mafuta, hivyo haina nafasi ya kuongeza bei katika eneo hilo.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mstaafu Profesa, Musa Assad, ni miongoni mwa wasomi wa masuala ya fedha aliyezungumzia tozo za sasa.

BURIANI MALKIA ELIZABETH II

# ‘Mama’ amefariki lakini Mfalme Uingereza akumbushwa haya

NA GAUDENSIA MNGUMI

MALKIA Elizabeth II wa Uingereza aliyefariki dunia juzi anatarajiwa kuzikwa Jumatatu ijayo Septemba 19, akiaga dunia na umri wa miaka 96, ana mengi mazuri na sifa kem kem, lakini wapo wenye jambo lao kwa ufalme aliouongoza kwa miaka 70.

Ni Malkia aliyedumu kwa muda mrefu zaidi akitawala kwa miongo saba au miaka 70, akielezwa kuwa hakuyumba katika kusimamia mila na desturi za Waingereza katika jukumu lake hilo.

Ameongoza nchi ikikabiliwa na changamoto lukuki huku kukiwa na mabadiliko makubwa ya kijamii na kiuchumi na kashfa ya familia iliyomhusu mwanae wa kwanza Mfalme Charles, aliyefikia hatua ya kuachana na mkewe Diana, ambaye haikuchukua muda mrefu alifariki kwenye ajali mbaya nchini Ufaransa.

Malkia ndiye aliyekuwa mkuu wa Uingereza katika kipindi cha kupigania uhuru Afrika ambayo, katika miaka ya mwanzo ya uongozi wake, alitoa uhuru kwa makoloni mengi.Hata hivyo, baadhi ya Waafrika wanamchukulia kuwa hakufanya juhudi za kutenda haki na kuisaidia Afrika ambayo inachukuliwa kuwa imechangia zaidi maendeleo ya Uingereza, Ulaya na Amerika.

Kwa mfano baadhi ya Wazimbabwe wanamkosoa kwa kushindwa kukuza maslahi ya Waafrika katika enzi ya uongozi wake. Kinachowauma ni suala la ardhi, wanakumbuka kuwa mwaka 1991, Malkia Elizabeth II alitembelea Zimbabwe kushiriki mkutano wa wakuu wa serikali wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola ambayo kwa ujumla ni makoloni ya zamani ya Uingereza.

Ni katika kipindi hicho Mugabe alitaka miongoni mwa mambo mengine, kutwaa ardhi na mashamba ya Wazungu bila kuwafidia na kuyagawa upya kwa Wazimbabwe wasio na ardhi. Hata hivyo, hilo lilikataliwa na halikuungwa mkono na Uingereza.

Jaribio la kujihusisha zaidi na serikali ya Uingereza kuhusu suala la ardhi lilifikia ukomo kwa kipingwa kila mahali na kuwekewa vikwazo vya kiuchumi hatua iliyoiangusha nchi hiyo hadi sasa,tena Uingereza ya Malkia ikimkataza Mugabe kukanyaga ardhi ya Malkia.

Kwa Zimbabwe Malkia ameacha mambo magumu na ikielekea kwake Mzimbabwe licha ya kuwa huru kisiasa, Uingereza haikufikiria kuhusu ardhi yake iliyopokonywa na wachache. Baadhi ya wanaharakati wa Umajumuni wa Afrika wanasema urathi (legacy)haiwezi kuzungumzwa bila kutaja unyonyaji na ubeberu ambao uliendelezwa barani Afrika na Waingereza.

Wanaona kuwa ufalme wa Uingereza sio taasisi tukufu, ni ufalme ambao Malkia Elizabeth aliuongoza na kuuwakilisha sio jambo la kusherehekewa kwa vile liliumiza na kutesa sana Afrika.



Mfalme Charles wa Uingereza na mama yake Malkia Elizabeth, aliyefariki wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

> “Ninamtarajia awe mwangalifu juu ya athari na changamoto za majukumu ambayo yametwishwa kwake kama Mfalme. Anapaswa kuwa mfano mzuri wa mama yake.

Kwa wanaharakati malkia na ufalme umekuwa ishara ya unyonyaji wa Waafrika, hasa ukandamizaji wa kikatili wa watu katika sehemu nyingine za dunia na ufalme huo ulihusika na udhalilishaji wa mtu mweusi.

### KUOMBA RADHI

Wanaamini Malkia Elizabeth alikuwa na nafasi na fursa za kurekebisha makosa haya kwa kukiri ukatili au kuomba msamaha kwa uovu, udhalilishaji na ukatili uliofanywa kwa himaya nyingi sio tu barani Afrika lakini pia Asia, Amerika ya Kusini na Karibiani.

Wanahisi kuomba msamaha na kulipa fidia kwa maovu hayo lingefaa kuwa jambo jema kwa kiongozi huyo, lakini alichagua kukaa kimya. Hilo lilikuwa chaguo lake, kupuuza.

Maoni kama hayo pia yanashikiliwa katika nchi zingine ikiwa ni pamoja na Afrika Kusini, ambayo ilivumilia miaka ya ubaguzi wa rangi, mateso , mauaji na udhalilishaji wa utu wa Mwafrika.

Chama cha upinzani cha Afrika Kusini cha Economic Freedom Fighters, kinasema katika taarifa yake kwamba wanachama wake hawaombolezi kifo cha malkia “Kwa sababu kwao kifo chake ni ukumbusho wa kipindi cha kutisha sana katika nchi hiyo na historia ya Afrika.”

Wapigania uhuru wa kiuchumi wanamkosoa Malkia Elizabeth kwa kukataa kukubali na kukiri kuwa halikuwa jambo jema ukatili wa ufalme wake, au kwa kuomba msamaha kwa makosa yaliyofanywa na ufalme huo sehemu nyingi duniani.

“Ikiwa kweli kuna maisha na haki baada ya kifo, Elizabeth na mababu zake wapate kile wanachostahili,” taarifa hiyo ya chama uhuru wa kiuchumi, inahitimisha.

Wanaoungana na Waafrika kuikumbusha Uingereza kuwa ina jambo la kufanya ni pamoja na Karen Attiah, mwandishi wa safu kwenye gazeti la The Washington Post.

Anaandika: “Watu weusi na brown (kahawia) kote duniani ambao walitendewa ukatili wa kutisha na kunyimwa haki za kiuchumi chini ya ukoloni wa Uingereza wanaruhusiwa kuwa na hisia tofauti na za kila namna kuhusu Malkia Elizabeth.

Mwandishi wa Kenya Shailja Patel, pia naye anasimulia jinsi ufalme wa Uingereza, ulivyokuwa wa kikatili chini ya utawala wa malkia huyo. Anaongeza: “Miezi 15 baada ya Malkia Elizabeth kuchukua uongozi wa ufalme eneo lote la Aberdares lilitangazwa kuwa ni shemu marufuku kwa Waafrika kuonekana. Amri ziliwekwa ili kuwapiga risasi na kuwaulia mbali Waafrika watakaoonekana mahali hapo.”

Anaendelea kusema kuwa baadhi ya manusura wa kubakwa, kuhasiwa, njaa, kutumikishwa kazi za kulazimishwa, na kuteswa katika koloni la Uingereza la Kenya bado wako hai.Hawakupata kamwe haki yao wala kuombwa msamaha waliotaka.” Anaandika Patel.

### KWA MFALME CHARLES

Rais wa zamani wa Ghana John Kufuor, anapoulizwa na Idhaa ya Kiswahili ya DW ni nini anachosema kuhusu ukosoaji wa Malkia Elizabeth, anasema “sitaki kuwakosoa watu kwa kile wanachofikiria. Ninakuambia kile ninachofikiria kuhusu Malkia, siendi kumwadhibu kwa dhambi za baba zake tangu zamani za kale.”

Ni kwamba dunia imepiga hatua zaidi hata baada ya ukatili wa siku za nyuma na kinachohitajika kwa sasa ni roho ya “kutangamana, inayozingatia na kuheshimu ubinadamu juu ya mmabo yote kama sababu ya lazima kwa kila jambo.”

Anasema kuwa kifo cha malkia, mtoto wake mkubwa Mfalme Charles III, Mkuu wa zamani wa Wales, sasa anaongoza nchi kama mfalme mpya. Pia anachukua nafasi kama mkuu na kiongozi wa mataifa ya Jumuiya ya Madola.

“Ninamtarajia awe mwangalifu juu ya athari na changamoto za majukumu ambayo yametwishwa kwake kama Mfalme. Anapaswa kuwa mfano mzuri wa mama yake,” Kufuor anamshauri mfalme mpya. **MITANDAO**

MFALME CHARLES III WA UINGEREZA...

# Auchukua ufalme bila kujali yaliyopita

## • Anaanza na 'jambo lao' ni athari kujitoa EU

**Na Mwandishi Wetu**

NI baba mzazi wa vijana wawili Harry na William lakini pia ni babu mwenye wajukuu watano, akiwa na miaka 73 anatangazwa rasmi kuwa ndiye Mfalme Charles III wa Uingereza na mataifa mengine 14 huru wanachama wa Jumuiya ya Madola.

Jumuiya hiyo ni muungano wa makoloni ya Uingereza yaliyoko Afrika, Amerika, Asia na Karibiani.

Majina yake kamili ni Charles Philip Arthur George, Prince (mkuu) wa Wales na kabla ya kifo cha Malkia Elizabeth II wa Uingereza, alikuwa mwana wa Mfalme na mzaliwa wa kwanza wa malkia huyo aliyefariki wiki iliyopita. Mfalme huyo amezaliwa Novemba 14, 1948.

Kwa mujibu wa Idhaa ya Kiswahili ya DW, Mwana wa Mfalme Charles III anatangazwa rasmi kuwa mfalme wa Uingereza katika hafla ya kihistoria iliyofanyika kwenye kasri la Mtakatifu James, jijini London.

Anachoahidi Mfalme mpya ni kwamba ataiga mfano wa mama yake, akisema ":Katika kuchukua majukumu hayo nitajitahidi kuiga mfano wa kutia moyo wa mama yangu katika kufuata na kudumisha katiba na kutafuta amani, maelewano na ustawi wa watu wa visiwa hivi, na ulimwengu wa Jumuia ya Madola duniani kote," ," anaahidi Mfalme Charles III.

Wanahabari wanamuelezea Mfalme Charles kama "mtu nyeti" (sensitive man) na mpenda mazingira, mtunza bustani mwenye bidii na anayefurahia kutunza bustani ya viumbe hai katika makazi yake huko mashambani.

Mfalme Charles III, pia anaaminika kuwa mchoraji stadi anayetumia rangi ya maji na ana mapenzi na mambo ya jadi kama kukata na kuweka ua kwa mtindo unaoitwa 'egde' eji, unaotengenezwa kwa kukata miti ilingane na kuvutia.

Akiwa kijana, wachambuzi wanasema hakuwa na uhusiano wa karibu na wazazi wake, ambao pengine kushirikiana nao kungeboresha hali yake kadiri alivyokuwa anakuwa na kuongezeka umri.



Mfalme Charles III wa Uingereza . **PICHA: MTANDAO**

> Kifo cha Diana kiliambatana na uvumi kuhusu uhusiano wa Prince Charles na mpenzi wa zamani Camilla Parker Bowles.

Ni msomi akihitimu katika vyuo vikuu vya Uingereza na Australia. Amesoma akiolojia, anthropolojia na historia katika Chuo Kikuu cha Trinity, Cambridge mwishoni mwa miaka ya 1960 kabla ya kuwa rubani wa Jeshi la Anga Uingereza (RAF).

Tangu mwaka 1970 amekuwa akihuduma kifalme tangu na alipofikia umri wa miaka 30 alifunga ndoa na Diana Spencer (19) mnamo 1981, katika harusi ya kifahari ya mwana wa mfalme iliyotazamwa na ambayo ilitazamwa na karibu watu milioni 800 duniani kote.

Alipata wana wawili wa Mfalme - Prince William, aliyezaliwa mnamo Juni 1982 na Prince Harry, Septemba 1984 , lakini wanandoa hao walitalikiana mnamo 1992 na ndoa kuvunjika rasmi.

Kifo cha Diana kiliambatana na uvumi kuhusu uhusiano wa Prince Charles na mpenzi wa zamani Camilla Parker Bowles. Ulisambaa na kuendelea baada ya talaka lakini 2005 waliokuwa wakizungumzwa wakajitokeza hadharani na kufunga pingu za maisha.

Charles amekabiliana na lawama nyingi na kukoselewa kwa miaka mingi, ikiwa ni pamoja na baada ya kifo cha Princess Diana katika ajali ya gari huko Paris 1996.

Wachambuzi wanasema kuwa kama mfalme mtarajiwa familia ya kifalme katika miaka ya hivi karibuni imefanya kazi ya kuboresha na hadhi yake kutokana na kuchafuka kutokana na visa mbalimbali.

Wanaongeza kuwa kumekuwa na juhudi za pamoja za kumsafisha Charles kutoka miaka ya 1980 na 1990, baada ya kifo cha Diana ambacho kilisababisha kudharauliwa na umarufu wake kushuka sana mbele ya jamii ambayo ilimpuuza.

Licha ya kuwa mwanzilishi na mlinzi wa mashirika kadhaa yakiwamo ya kusaidia wajasiriamali wachanga, kuhifadhi mazingira asilia na hata yaliyotengenezwa na wanadamu mara nyingi kura za maoni zilionyesha kuwa umaarufu wake uko chini ikilinganishwa na malkia (mama yake mzazi ) na mtoto wake Prince William.

Waingereza wanasema kuwa katika suala la kuwa mfalme wa nchi ni lazima uwe na aina ya utulivu, usipendelee wala kuegemea upande wowote na hilo halijaonekana au sifa hizo kwa Charles bado hazijaonekana.

Amesema jambo muhimu zaidi kwake litakuwa kuwajali na kuwahudumia watu na kutoa aina fulani ya uongozi, hivyo Waingereza wanaokuwa na utayari wa baadhi ya dalili za sifa za uongozi atakazoleta kwenye nafasi hiyo.

Mfalme Charles anaingia kwenye kasri lake akianza kupambana na jambo kuu la Uingereza kusimama kama mtoto yatima baada ya kujiondoa kwenye uhusiano wa miaka 50 na Umoja wa Ulaya (EU).

Imetoka kwenye soko la EU pamoja na umoja wa forodha. Kazi bado ipo, mambo ni magumu na katika muda mfupi mawaziri wakuu wawili wameondoka madarakani wa kwanza Teresa May na sasa Boris Johnson.

**MITANDAO**

# Ofisi ya Msajili yahofiwa pengine haiko huru, wadau wataka katiba kunusuru

**INATOKA UK. 11**

Na ninaamini kwamba atashindwa kumbeba Lipumba na kutoa hukumu sahihi," anasema.

Anashsuri kuwa, kwa uhai wa demokrasia ndani ya vyama vya siasa, ingekuwa vyema iwapo msajili angetoa uamuzi kuhusu mgogoro wao, ili wajue wako upande gani, wajue hatua za kuchukua.

Msajili huyo Jaji Francis Mutungi, akizungumzia madai hayo, anakiri kwamba migogoro hiyo ipo ofisini kwake, ambapo anawataka wadau kuipa muda ofisi yake ili hatimaye itoe uamuzi badala ya kushinikizwa.

"Ofisi yangu inafanya kazi kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria, sio shinikizo, hivyo hao wanaolalamika, wanatakiwa kuwa wavumilivu na kuacha malalamiko yasiyo na msingi," anasema Jaji Mutungi.

Jaji Mutungi anasema, anajua ofisi yake inaweza kuzushiwa mambo mengi yasiyo na msingi, na kwamba itaendelea kuwa mlezi wa vyama vya siasa na kusimamia haki bila kushinikizwa.

Msajili huyo anasema suala la kujipa muda kushughulikia migogoro ni la muhimu, na kwamba kinachotakiwa ni uvumilivu badala ya kutaka kulazimisha mambo ambayo yanahusu sheria.

**MGOGORO NCCR**

Mwaka huu, Mjumbe wa Halmashauri Kuu na Mwenyekiti wa azimio la kumwengua Mwenyekiti James Mbatia, Joseph Selasini, anatangaza uamuzi wake unaoambatana na kuvunjwa kwa Baraza la Wadhamini la NCCR- Mageuzi.

Katika uamuzi huo, wanateuliwa wajumbe wapya ambao watasajiliwa kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa, huku Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, akikiri kupokea barua kutoka NCCR-Mageuzi kuwa kuna mabadiliko ya wajumbe wa bodi ya wadhamini.

Baada ya tamko hilo, ndipo muda mfupi baadaye Katibu Mkuu wa NCCR-Mageuzi, Martha Chiomba, alifunga ofisi za chama hicho zilizopo Ilala, Dar es Salaam, ili kumzuia James Mbatia kujihusisha na shughuli za chama.

Kufuatia tukio hilo, wanachama wanaomuunga mkono Mbatia, walifika ofisini hapo na kuzungumza na wanahabari wakisema waliotangaza kumsimamisha kazi hawana mamlaka na pia akidi haikutimia.

Tukio hilo lilimwibua Katibu Mwenezi Edward Simbeye, aliyepinga kilichofanyika akidai ni uhaini na uhuni ndani ya chama na kusema hakiwezi kukubalika, na kwamba chama kitakaa na kufanya maamuzi mengine.





## Wanafunzi washindwa kufanya mitihani 2021

Na Magdalena Jackson, SJMC

WATOTO 4,419 wa darasa la nne hawakufanya mitihani mwaka uliopita kutokana na kuacha shule katika wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

Akizungumza hayo juzi wilayani humo, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga, alisema: "Tusipowafuatilia watoto hawa tunakwenda kutengeneza jamii ambayo ina wakola wengi sana kwa sababu ya kutokuwafuatilia watoto wanaoacha shule."

Alisema mkoa wa Dodoma haukutumia vizuri fursa iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwataka watoto wote walioacha shule kupata nafasi ya kurudi tena shuleni, ambapo wanafunzi wengi wa mkoa huo hawakurudi shule.

Mganga alisema wanafunzi wa darasa la saba 1,329 hawakufanya mitihani ya majaribio (mock), hivyo kuna uwezekano wa kutokufanya mtihani wa mwisho na kwa upande wa kidato cha nne, wanafunzi 492 sawa na asilimia 11.3 hawakufanya mtihani wa mock.

"Tunao mradi wa shule bora ambao unatupatia fedha ya kujenga miundombinu kutegemea na utekelezaji wa vigezo ikiwamo wanafunzi kudumu shuleni kuanzia darasa la kwanza hadi la saba pamoja na kiwango cha watoto waliofanikiwa kujiunga na kidato cha kwanza," alisema.

Alisema, idadi ya wanafunzi wanaoacha shule inavyoongezeka inasababisha kukosa fedha za mradi kwa ajili ya kutatua adha ya miundombinu iliyopo wilayani hapo kwa kuwa wanafunzi wanashindwa kudumu shuleni.

Mganga aliuomba uongozi kufanya mkakati wa kuanzisha kampeni maalum itakayosaidia kuwarudisha shuleni wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali kama vile mimba na utoro.

# Vijana waonywa kuhusu suala 'kumwagilia moyo'

Na Augusta Njoji, DODOMA

MKURUGENZI Msaidizi wa Magonjwa Yasiyo ya kuambukiza katika Wizara ya Afya, Dk. James Kiologwe, amesema mtindo wa maisha ulioibuka hivi karibuni, unaotumiwa na vijana maarufu kama 'kumwagilia moyo', unachochea kunywa pombe kupita kiasi.

Dk. Kiologwe amesema tabia hiyo inawaweka kwenye hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari.

Aliyasema hayo jana alipoulizwa swali na mwandishi aliyetaka kujua namna vijana walivyo kwenye hatari ya magonjwa hayo, katika kikao cha waratibu wa mikoa wa magonjwa hayo na waandishi wa habari kilichofanyika kwa njia ya mtandao.

Kwa mujibu wa Dk. Kiologwe, matumizi ya pombe kupita kiasi ni kichocheo cha magonjwa hayo.

Aidha, alisema kuna asilimia 18 ya vifo vya mapema kwa watu wenye miaka 30 hadi 60 na kwamba hali hiyo inatokana na mtindo wa maisha wanaoishi.

"Hivi sasa nchini magonjwa haya yanachangia takribani asilimia 41 ya vifo vyote vinavyotokea kila mwaka na ni gharama kubwa kuyatibu, vijana mna tabia nyingi ngumu, siku hizi mnatumia msemo wa kumwagilia moyo ni changamoto nyingine ambayo inawaweka watu wengi kwenye hatari ya kuishia kupata magonjwa haya," alisema.

Alibainisha kuwa utafiti unaonyesha kuwa watu milioni 15 duniani wanakabiliwa na kiharusi, asilimia nane wanaishi Afrika na kiharusi pekee huchangia asilimia 85 ya vifo vinavyotokea kila mwezi kutokana na tatizo hilo barani Afrika.

Pia alisema Tanzania utafiti unaonyesha asilimia 26 ya watu wana shinikizo la damu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili asilimia 33 ya wagonjwa wanaopokea wana kiharusi na hufa ndani ya mwezi mmoja tangu wamepokelewa.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mpango wa Taifa wa Kuzuia Magonjwa hayo, Goodluck Tumaini, alisema kutokana na hali hiyo wizara imeona waje na mkakati wa kufikia jamii kupitia waandishi watakaoshirikiana na waratibu kusaidia kutoa elimu ya kuepuka magonjwa hayo.



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa (kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DUWASA yajipanga kero ya majitaka

Na Peter Mkwavila, DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), imetaja mikakati ya kukabiliana na kero ya majitaka kwenye baadhi ya mitaa ikiwamo inatarajia kufanya maboresho makubwa baada ya kupata mkopo wenye masharti nafuu utakaogharimu Sh. bilioni 163.

Akizungumza jana na Nipashe, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa DUWASA, Edwin Mwijage, alikiri kuna tatizo la majitaka kwenye baadhi ya mitaa na mamlaka hiyo inalishughulikia.

Alisema serikali ya Korea imetoa mkopo huo na wako kwenye hatua za mwisho ya kumpata Mhandisi Mshauri.

"Mtandao wa majitaka Makole ni wa zamani unahitaji maboresho ili kuendana na ongezeko la watu. DUWASA tunatarajia kutekeleza mradi mkubwa sana wa majitaka na tutafikia kata 11 mpya na 14 za zamani," alisema.

Alisema maeneo ya kuboresha ya mtandao wa majitaka yatakuwa yenye urefu wa kilometa 257.

"Huu mradi mabwawa 16 ya kutibu majitaka yatajengwa eneo la Nzuguni ambapo serikali ilishalipa fidia kwa wananchi takribani Sh. milioni 600," alisema. Mwijage alisema kuwa mhandisi mshauri wa mradi anatarajiwa kupatikana mwishoni mwa mwezi huu.

"Mradi utatekelezwa kati ya miaka mitatu hadi mitano, unajua tatizo lililopo kwenye maeneo ambayo jioni yanatiririsha majitaka au kutoa harufu ni matumizi yasiyo sahihi ya mtandao wa majitaka," alisema.

Alifafanua kuwa mtandao umesanifiwa kupitisha majitaka lakini wananchi wanatupa taka ngumu kama nguo, taulo za kike, pampasi, mipira ya kiume hasa kwenye vyumba za kulala wageni.

"Pia wanachepusha maji ya mvua kwenye mtandao wa majitaka hali inayosababisha mchanga kujaa na kuziba. Tunashauri wananchi wazingatie matumizi sahihi ya mtandao wa majitaka kama ilivyoelezwa kwenye mkataba walipojiunga," alisema.

"Wizi wa mifuniko ya chemba za majitaka unasababisha taka ngumu kutupwa na kusababisha kufurika kwa majitaka," aliongeza na kusisitiza watumie mtandao huo kwa matumizi yaliyoelekezwa.

Nao baadhi ya wananchi wa Makole walisema baadhi ya wenye nyumba ikiwamo nyumba za kulala wageni wamekuwa wakitiririsha maji machafu barabarani kutokana na kukosa miundombinu.

Juma Sangali, alisema wanalazimika kufanya hivyo baada ya kukosa miundombinu ya mifereji inayosafirisha maji hayo machafu kutoka kwenye nyumba zao hadi kwenye bomba kubwa.

Naye Agness Yohana, alisema mifereji iliyopo ni ya muda mrefu, pia kwa hivi sasa baadhi ya wakazi wameamua kutupia takataka na kusababisha kuziba na ndiyo maana wanatiririsha maji hayo machafu mtaani hapo.

Mkai mwingine, Mathayo Yona, alisema tatizo lililoko mtaa wa Mahakamani kwenye kata hiyo ni nyumba kutokuwa na makalo na vyoo vilivyo vingi vimejaa na havijaunganishwa na mfumo wa majitaka.





Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari kutoka Zanzibar, waliokwenda mkoani humo, kwa ajili ya kujifunza mbinu za kuongeza ufaulu kwenye mitihani ya kitaifa, katika mkutano uliofanyika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Loleza jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mpango ampa kibarua Jafo kuhusu miti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amemwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Selemani Jafo, kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kila halmashauri nchini kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka ili kujiridhisha kama yametekelezwa ipasavyo.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo juzi jijini hapo alipofungua Mkutano wa 36 wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) huku akibainisha kuwa kuna mizaha mingi inafanyika kwenye utekelezaji wa mpango huo wenye lengo la kutunza mazingira nchini.

Alisema kuna uwezekano baadhi ya halmashauri zinapanda miti hiyo lakini haziihudumii wala kuilinda, hivyo kusababisha ife au iliwe na wanyama jambo ambalo alisema litasababisha mpango huo kutokuwa na mafanikio.

"Hapa kuna mizaha mingi inafanyika. Ukifuatilia unakuta hiyo miti ambayo inapandwa kila mwaka haipo. Sasa hii itatusababishia kuwaachia watoto na wajukuu zetu taifa ambalo halina uendelevu wa mazingira au bionuai," alisema.

Pia alikemea baadhi ya viongozi wa chama na serikali wanaojihusisha na uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na kupokea rushwa ili kuruhusu mifugo kuingia kwenye maeneo ya hifadhi pamoja na vyanzo vya maji.

Alisema kwenye baadhi ya maeneo nchini, baadhi ya viongozi hao wamediriki kushawishi wananchi kuvamia kambi za vyombo vya ulinzi, hivyo akawataka madiwani kuwakemea bila woga. Katika hatua nyingine, Dk. Mpango aliiagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuongeza kasi ya upimaji na upangaji wa miji na majiji nchini ili kuendana na kasi ya ongezeko la watu kwenye maeneo hayo pamoja na kurahisisha upatikanaji wa huduma za jamii.

Pia aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kushirikiana na madiwani kusimamia upimaji wa viwanja vya makazi na utoaji wa vibali vya ujenzi ili kuhakikisha miji inakuwa katika hali yenye mpangilio mzuri wa makazi.

"Lakini kwenye maeneo ya miji yetu hasa maeneo yenye mikusanyiko, mwende mkaweke vitunza taka ili wananchi wanaozalisha taka wazihifadhi humo badala ya kuzitupa ovyo na kuifanya miji yetu kuwa michafu," alisema Dk. Mpango.

Mwenyekiti wa ALAT, Murshid Ngeze alisema jumuiya hiyo imeongeza ushirikiano na jumuiya mbalimbali za kimataifa ikiwamo Jumuiya ya Serikali ya Mitaa Afrika na kwamba tayari wameshaanza kunufaika.

Alisema ushirikiano huo umeanza kuuza matunda kwa maelezo kuwa wameanza kupata ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo inayohusu mazingira, afua na elimu.

Halmashauri zetu zitaomba ufadhili kwenye miradi mbalimbali ambapo zitachangia asilimia 30, halmashauri rafiki ya Morocco itachangia asilimia 10 na mfadhili atachangia asilimia 60 kwa hiyo naziomba halmashauri zetu ziendelee kuomba," alisema Ngeze.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema ofisi yake itaendelea kushirikiana na halmashauri kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

## Furaha ujio wa mradi wa maji

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

ZAIDI ya kaya 8,000 za Kijiji cha Mpandapanda, Kiwira wilayani Rungwe zimeanza kunufaika na mradi wa maji wenye thamani ya Sh. milioni 500.

Mradi huo unazalisha lita milioni 19 kwa siku na umetekeleza kwa kutumia fedha za mpango maendeleo na mapambano dhidi ya UVIKO - 19 na umejengwa kwa kutumia akaunti ya dharura (Force account).

Akizungumza baada ya kukagua na kuzindua tangi la maji lenye uwezo wa kuhifadhi lita 135,000, Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa 2022, Sahili Nyazabara, alisema miradi inayotekelezwa na Wakala wa Maji Vijijini (Ruwasa) ni fursa kwa wananchi.

Tangi hilo lililozinduliwa na Nyanzabara linatarajiwa kusambaza maji katika vituo 16 vilivyosambazwa katika maeneo ya vijiji vinavyozunguka eneo hilo.

"Ni vizuri mkawa mnawapa wananchi elimu ili kuwa na utaratibu wa kulipa ankara za kila mwezi ili ziweze kuboresha miundombinu iliyo haribika," alisema Nyazabara.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia jamii kupata huduma bora na kuchochea shughuli za kiuchumi hususan kilimo cha mboga.

Naye Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliwataka wananchi wa Kata ya Kiwila kutoendelea na shughuli za kibinadamu kwenye chanzo cha maji.

# Madereva serikali waonywa ukiukaji sheria

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, limewatangazia kiama madereva wa magari ya serikali wanaokiuka sheria za usalama barabarani kuwa litawakamata na kuwachukulia hatua za kisheria kama ilivyo kwa madereva wa magari mengine.

Mkuu wa Kikosi hicho nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, alitoa tahadhari hiyo juzi alipotembelea eneo la mteremko wa Inyala nje kidogo ya Jiji la Mbeya mahali zilipotokea ajali za mfululizo hivi karibuni na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 30.

Lengo la ziara hiyo ilikuwa kukagua maendeleo ya ujenzi wa maeneo ya maegesho ya magari kwenye eneo la Inyala ambako umeanzishwa utaratibu wa malori na magari madogo kupita kwa awamu pamoja na barabara ya mchepuko yenye urefu wa kilomita 2.5.

Alisema madereva hao watachukuliwa hatua hata kama wakati wanaendesha magari hayo watakuwa wako na viongozi bila kujali ukubwa wa kiongozi husika na kwamba lengo la utaratibu huo ni kupunguza ajali.

Mpaka sasa, alisema askari wa usalama barabarani wameshapewa maelekezo ya namna ya kuwashughulikia madereva hao kwa kuzingatia sheria na miongozo ya kazi yao.

"Askari wetu wa usalama barabarani tayari tumeshawapatia maelekezo ya namna ya kushughulika na hawa madereva. Endapo yuko na 'bosi' wake atasimamishwa na askari atamfuata huyo kiongozi na kumpa maelezo kwamba aliyekiuka sheria ni dereva wake na anastahili kuchukuliwa hatua," alisema Mutafungwa.

Pia alisema jeshi hilo linaanzisha ukaguzi maalumu wa mifumo ya malori katika vituo vya ukaguzi vilivyopo kwenye miji ya Tunduma mkoani Songwe na Makambako mkoani Njombe.

Alisema ukaguzi huo pia ni sehemu ya mikakati ya kupunguza ajali za barabarani kwa maelezo kuwa malori mengi ambayo yanasababisha ajali hasa kwenye maeneo ya miteremko huwa yanasababishwa na kuwa mabovu kwenye mifumo ya breki.

Kwa mujibu wa Mutafungwa, lori lolote litakalokaguliwa kwenye vituo hivyo na kubainika kuwa bovu, halitaruhusiwa kuondoka kwenye kituo mpaka lifanyiwe matengenezo na kwamba ili kuyadhibiti malori hayo watakuwa wanayaondoa namba.

Aliwataka wamiliki na wasimamizi wa malori kuhakikisha wanayafanyia matengenezo magari yao ili kuepuka kukumbana na kadhia ya kuzuiwa kuendelea na safari yatakapokaguliwa.

Kamanda Mutafungwa alisema ukaguzi huo pamoja na kwamba unaweza ukasababisha kero lakini una lengo zuri la kuokoa maisha ya watu ambao wamekuwa wakifariki kwenye ajali zinazosababishwa na malori hayo.

Kuhusu utaratibu wa magari makubwa na madogo kupita kwa awamu kwenye mteremko wa Inyala, Kamanda Mutafungwa alisema utasaidia kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara.

"Ni kweli utaratibu huu utaleta usumbufu kidogo kwa wasafiri lakini lengo lake ni zuri maana tunalenga kuokoa maisha yao pamoja na vyombo vyenyewe kwa hiyo nawaomba wawe wavumilivu," alisema Mutafungwa.

Agosti 11, mwaka huu, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango alitembelea eneo la mteremko huo wa Inyala na kutoa siku 10 kwa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) kukamilisha ujenzi wa kituo cha magari kusubiriana.





# Bil. 16/- kukarabati nyumba zilizojengwa na Karume

**Na Rahma Suleimman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuzifanyia ukarabati nyumba za maendeleo ambazo zilijengwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, serikali imesema imetenga Sh. bilioni 16 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba hizo ambazo kwa sasa zipo katika hali mbaya ya uchakavu.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Juma Makungu jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, Hassan Hamad Omar, aliyetaka kujua lini ukarabati mkubwa wa nyumba za maendeleo utafanyika.

Makungu alikiri nyumba nyingi kuwa katika hali mbaya ya uchakavu kwa sababu zimejengwa miaka mingi bila ya kufanyiwa matengenezo muhimu.

Alisema kupitia fedha za Mfuko wa Shirika la Nyumba la Zanzibar, imetenga Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za Pemba.

Alizitaja nyumba za Micheweni, Mtemani pamoja na Kengeja, Pemba kuwa katika hali mbaya na zinahitaji ukarabati mkubwa.

"Tutazifanyia ukarabati mkubwa nyumba za maendeleo ziliopo Unguja na Pemba ambazo zipo katika hali mbaya za uchakavu wake kiasi ya kutishia maisha ya wapangaji wake," alisema.

Makungu aliwataka wapangaji wa nyumba hizo kuhakikisha wanalipa kodi ya mwezi ambayo itatumika kwa ajili ya ukarabati huo.

Alisema moja ya changamoto kubwa inayozikabili nyumba hizo ni wapangaji kushindwa kulipa kodi ya mwezi na matokeo yake kusababisha malimbikizo ya muda mrefu.

"Wizara inatoa agizo kwa wapangaji wote kuhakikisha wanalipa madeni yao ambayo yatatumika kwa ajili ya kuendesha shughuli za shirika ikiwamo ukarabati," alisema.

**"Tutazifanyia ukarabati mkubwa nyumba za maendeleo ziliopo Unguja na Pemba ambazo zipo katika hali mbaya za uchakavu wake kiasi ya kutishia maisha ya wapangaji wake," alisema.**

# SMZ kuziingiza kaya maskini Mfuko Maendeleo ya Jamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema ipo katika hatua za mwisho kuzitambua kaya maskini ambazo zitaingizwa katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) awamu ya tatu.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma, wakati akiwasilisha taarifa ya mfuko huo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, ambao kwa sasa upo katika hatua za mwisho kuzitambua kaya maskini kuingizwa katika mpango wa tatu.

Alisema mfuko huo ambao unaingia awamu ya tatu hautamwacha mtu au kumtambua katika mpango huo kwa waliofikia sifa.

"Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) upo katika awamu ya tatu ya kuzitambua kaya maskini kwa kufanya upembuzi yakinifu ambapo tunawahakikishia wajumbe kwamba hakuna mtu mwenye sifa atakayeachwa bila ya kuingizwa au kutambuliwa," alisema.

Aidha, alisema mfuko huo umepata mafanikio makubwa tangu kuanzishwa kwake ikiwamo kuzikomboa kaya maskini kiasi cha kuendesha maisha na kusomesha watoto wao shule.

"Mafanikio ya mpango wa kunusuru kaya maskini, Tasaf, awamu ya kwanza yanaonekana wazi wazi ni kuwafikia walengwa katika familia ambazo zimepata kuendesha maisha yao kwa ufanisi mkubwa," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya viongozi wakuu wa kitaifa, Machano Othman Said, alizipongeza serikali zote mbili kwa kutekeleza kwa dhati mpango huo ambao umelenga kuondokana na umaskini.

Aliitaka Serikali ya Zanzibar kuhakikisha mpango huo unazifikia kaya zote zenye sifa ili kwenda sambamba na malengo ya kuondokana na umaskini.

"Wito wangu tunataka kuona kwamba mpango wa kunusuru kaya maskini awamu ya tatu unazifikia kaya zote zenye sifa," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia taarifa ya kamati ya viongozi wakuu wa kitaifa, walisema lazima Tasaf awamu ya tatu iwafikie hadi vijijini na kuhakikisha watoto wanaoishi katika mazingira magumu wanawezeshwa na kurudi shule.

"Tunakabiliwa na changamoto kubwa zaidi vijijini wapo watoto wengi wameacha shule wakijiingiza katika ajira ngumu ambapo tunataka Tasaf iwafikie haraka na kuwarudisha shule," alisema Bihindi Hamad Khamis, Mwakilishi Viti Maalumu Wanawake, Pemba.




Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Muhamed Said (kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali: Mwongozo kudhibiti biashara vyuma chakavu upo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, amesema serikali imeweka mwongozo utakaosaidia kudhibiti biashara ya vyuma chakavu kwa ajili ya kuepusha athari za uharibifu wa miundombinu ya serikali.

Alisema hayo, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, aliyetaka kujua serikali haioni sababu ya kusitisha biashara ya vyuma chakavu kutokana na kuwapo kwa kasi ya athari za miundombinu ikiwamo ya barabara na majisafi na salama.

Shaaban alisema hakuna sababu ya kupiga marufuku biashara hiyo kutokana na athari za uharibifu wa mazingira ya miundombinu kwasababu mwongozo uliowekwa unafanya kazi vizuri.

Alisema biashara ya vyuma chakavu ina tija kutokana na mapato inayopata serikali katika usafirishaji na kutoa ajira kwa wananchi ikiwamo wafanyabiashara wanaosafirisha nje ya nchi.

Pia wafanyabiashara wote wanaofanya biashara hiyo wana vibali vinavyowezesha kufanya biashara hiyo kwa mujibu wa sheria.

Kadhalika, serikali itahakikisha mwongozo uliowekwa katika kusimamia biashara ya vyuma chakavu inasimamiwa kikamilifu ili kuepuka uharibifu unaofanywa na watu wasiokuwa waaminifu na kusababisha hasara kwa taifa.

Alisema jumla ya tani za vyuma chakavu 12,385 zimesafirishwa kwa mwaka 2021-2022 na 6,243 zimesafirishwa katika mwaka 2021 huku 6,142 zikisafirishwa mwaka 2022.

"Kazi yetu kubwa ni kuhakikisha miongozo yote iliyowekwa inatekelezwa na kufuatwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

# ‘Panya road’ 116 mbaroni Dar

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia watuhumiwa 116 wanaodaiwa kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa nyumba na kupora mali mkoani humo.

Kaimu Kamanda wa Kanda hiyo, William Mkonda (pichani), aliyasema hayo jana na kueleza kuwa watuhumiwa hao wamekamatwa katika msako uliofanyika kwa siku tatu maeneo mbalimbali mkoani humo ulioanza Jumamosi iliyopita.

Alisema watuhumiwa hao wamekamatwa wakiwa na vielelezo mbalimbali zikiwamo silaha za jadi ambazo ni panga, visu na vifaa vya kuvunjia nyumba.

“Operesheni hii inayoongozwa na taarifa za siri dhidi ya uhalifu na wahalifu katika maeneo mbalimbaji jijini Dar es Salaam, inafanywa usiku na mchana dhidi ya mtu au kikundi cha kihalifu, uvunjaji wa nyumba na uhalifu mwingine,” alisema.

Alisema Jeshi la Polisi linawaomba wananchi kuendelea



kushirikiana nao kutoa taarifa za kuwabaini watu wa aina hiyo.

Pia, jeshi hilo limewataka viongozi wa serikali za mitaa kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi katika mitaa yao.

Katika hatua nyingine, Kamanda Mkonda alisema wamefanikiwa kukamata silaha aina ya rifle iliyokatwa mtutu ikiwa na risasi mbili eneo la Mwasonga, Kigamboni.

Alisema juzi usiku katika kijiji cha Morogoro, Mkuranga, Mkoa wa Pwani, watuhumiwa wa ujambazi watano wakiwa na silaha walimjeruhi mfanyabiashara wa duka la vifaa vya ujenzi na miamala ya fedha, Denis Komba (23), na kumpora fedha Shilingi milioni mbili na simu ndogo ya mkononi.

Alisema katika uchunguzi walibaini watuhumiwa hao walikuwa wakielekea Mwasonga na katika mtego wa Jeshi la Polisi, walibaini wanafuatiliwa na kutupa begi lililokuwa na silaha na kutokomea porini.

# Maji ya maiti yadaiwa kusababisha kansa

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema maji ya kuoshea maiti na dawa za kuhifadhia samaki ni moja ya visababishi vya ugonjwa wa saratani.

Dk. Mpango (pichani) alitoa tahadhari hiyo jana jijini hapa wakati wa uzinduzi wa wodi ya wagonjwa wa saratani katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando. Jengo hilo lenye ghorofa tatu, limejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 5.6.

Alisema hayo yalibainika kupitia utafiti wa awali uliofanywa na watalaam kuanzia mwaka jana unaoonyesha kuwa maji hayo yanatumiwa na wavuvi kuvulia samaki na dawa za kuhifadhia samaki vinasababisha saratani.



Pia aliwataka Watanzania kuepuka matumizi ya pombe, tumbaku na kuhakikisha wanafanya mazoezi ili kupambana na ugonjwa wa saratani huku akiweka bayana kwamba saratani ikigundulika mapema, inatibika na kupona, hivyo wananchi wanatakiwa kufika hospitalini badala ya kudhani wamerogwa na kwenda kwa waganga.

Aliwapongeza wafanyakazi wa hospitali ya Bugando kwa kuchangia Sh. milioni 250 pamoja na wadau wengi walitoa Sh. milioni 450 kwa ajili ya kujenga jengo hilo.

Dk. Mpango aliiagiza Wizara ya Afya kutoa Sh. bilioni 3.1 Kwa ajili ya kununulia mashine ya kusaidia matibabu ya saratani na fedha za kufanyia utafiti zinazofikia Sh. milioni 500.

Mkurugenzi Mkuu wa Bugando, Dk. Fabian Masaga, alisema Tanzania kuna wagonjwa 45,000 na kati ya hao chini ya asilimia 45 wanafika hospitalini wakiwa wamechelewa.

Aliongeza kuwa Kanda ya Ziwa inaongoza kwa kuwa na wagonjwa wa saratani na kwamba watalaam wamechukua sampuli za damu kutoka kwa wananchi wa mikoa minane ili kufanya utafiti kwa nini eneo hilo linaongoza kwa ugonjwa huo.

Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mwanza, Renatus Nkwande, alisema ujenzi huo ulikuwa wa awamu mbili na ule wa kwanza ulikamilika mwaka 2013 na jana walikamilisha awamu ya pili na kuzinduliwa.

Alisema licha ya kukamilisha ujenzi huo na kuweka vifaa, lakini bado mashine za kupima wagonjwa hazitoshi nakuomba serikali kuendelea kusaidia ili kumaliza shida hiyo.

Pia alisema bado kuna uhaba wa watalaam katika hospitali hiyo ambayo ilijengwa na kanisa katoliki mwaka 1971 na kuhudumia mikoa minane hapa nchini.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema serikali imepeleka mkoani Mwanza Sh. bilioni sita kwa ajili ya kununulia dawa na kwamba Hospitali ya Bugando imepewa mashine ya MRI yenye thamani ya Sh. bilioni 2.1 ili kuhakikisha huduma zinaendelea kuboreshwa.

Dk Mpango pia alizindua jengo la Sh. bilioni 10 na stendi ya Nyamhongolo iliyogharimu Sh. bilioni 26.

Pia jana alizindua jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza ya Sekou Toure lililojengwa kwa Sh. bilioni 10 na stendi ya mabasi ya Nyamhongolo iliyojengwa kwa Sh. bilioni 26.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 27-07-2021

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Kampuni ya **PMM ESTATES (2002) LTD** itasafirisha mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Kurasini Dar es salaam kwenda Handeni Tanga** kwa kutumia gari zenye namba za usajili **T283DQV/T124DJK, T864CVX/T472CVG, T904CVX/T473CVG, T274DQV/T472CVG na T281DQV/T473CVG.**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 18**
   **Upana - mita 3.25**
   **Kimo - mita 4.8**

   Safari imepangwa kuanza tarehe 13.09.2022

3. Njia zitakazotumika ni Bandari Road, Kilwa Road, Mandela Road, Nyerere Road, Bagamoyo and Msata.
   Gari zitasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza*



**KUPOTEA KWA CHETI**



**JOHN EMANUEL NKONGOLO a**natangaza kupotelewa na Cheti cha **DIPLOMA IN HUMAN RESOURCE MANAGEMENT** Chenye **NO. 3110096/T.12** kilichotolewa na **MZUMBE UNIVERSITY-MBEYA CAMPUS COLLEGE** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya Polisi: DOD/DOD/RB/363298/2022.**



**KUPOTEA KWA CHETI**



**MATHEW KAIZILEGE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0836-0127** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KILUVYA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2007.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA. MR/RB/8949/2014**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KILINDI**

**MAOMBI MADOGO NA. 11 YA MWAKA 2022**
**LUSANE VILLAGE……………….MSHINDA TUZO**
**DHIDI YA**
**CHARLES DALUSI………………… MSHINDWA TUZO NA.1**
**KWA MSHINDWA TUZO, CHARLES DALUSI,**

**POPOTE PALE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
Lusane village wameleta maombi dhidi yako mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) kilindi-Tanga lililopo Songe. Maombi haya yamepangwa kusikilizwa tarehe 22/09/2022 saa tatu asubuh mbele ya Mh.E.R Mhina Mwenyekiti.
Hivyo basi unatakiwa kufika wewe mwenyewe au wakili wako kwa tarehe iliyopangwa. Vielelezo kuhusu shauri hili vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Kilindi, Endapo hautatekeleza haya shauri hili litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Kilindi leo tarehe 12/09/2022


**MHINA ER**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KILIDNI**




## HABARI KIMATAIFA

# Ruto aapishwa, Samia ampongeza

Na Maulid Mmbaga



Rais William Ruto akiapishwa na Msajili Mkuu wa Mahakama, Anne Amadi (kushoto), huku Jaji Mkuu, Martha Koome (hayupo pichani), akishuhudia tukio hilo lililofanyika jana Uwanja wa Kasarani, Kenya. **PICHA: MTANDAO**

WILLIAM Ruto jana aliapishwa rasmi kuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Kenya huku Rais Samia Suluhu Hassan akiwapongeza wananchi wa nchi hiyo kwa kufanya uchaguzi wa amani.

Sherehe za kuapishwa kwa Ruto, ambaye kabla ya kuwa Rais alikuwa Naibu Rais zilifanyika jijini Nairobi na kuhudhuriwa na maelfu ya wananchi waliojitokeza pamoja na marais na wakuu wa nchi kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika.

Kutokana na kuingia Ikulu kuongoza taifa hilo la Afrika Mashariki, Ruto kijana kutoka kijiji cha Kamagut, Kaunti ya Uasin Gishu, ameweka rekodi ya kutoka Naibu Rais hadi mkuu wa nchi.

Ruto aliapishwa katika Uwanja wa Michezo wa Kasarani baada ya kushinda uchaguzi wa urais kwa kura milioni 7.1 huku mpinzani wake Raila Odinga akipata milioni 6.9. Odinga hakuhudhuria sherehe za kuapishwa kwa Ruto.

Akihutubia mamia baada ya kushika wadhifa huo, Rais Ruto aliwashukuru waliowezesha kufanikisha ushindi huo, huku akimshukuru mtangulizi wake, Uhuru Kenyatta, kwa kukubali na kuungana naye kufanikisha jambo la kikatiba.

Pia aliipongeza Tume Huru ya Mipaka na Uchaguzi nchini (IEBC), mahakama na wapigakura kwa uchaguzi mzuri, huku akiwashukuru kwa kuwachagua magavana saba wanawake, pamoja na idara za usalama kwa kukataa kila jaribio la kudhoofisha matakwa ya wananchi na kuahidi kufanya kazi na kila mmoja.

"Ili kudhihirisha zaidi dhamira yangu ya uhuru wa mahakama, mchana wa leo (jana) nitawateua majaji sita ambao tayari wamependekezwa kwa ajili ya kuteuliwa katika mahakama ya rufani ambayo yalifanyika miaka mitatu iliyopita. Kesho (leo) nitaongoza kuapishwa kwao ili waendelee na shughuli ya kuwahudumia Wakenya," alisema.

Naye Naibu Rais, Rigathi Gachagua, alisema siku za hofu zimekwisha na kwamba wako huru kuzungumza na kutoa maoni yao kwenye makundi songezi, bila kuhofia kurekodiwa na kuchukuliwa hatua.

**SAMIA APONGEZA**

Akihutubia hadhara hiyo, Rais Samia Hassan alimpongeza kiongozi huyo na Wakenya kwa uchaguzi na kusimamia amani wakati wa mchakato mzima hadi kuapishwa kwake.

Aidha, aliwataka Wakenya kushikamana katika kujenga nchi yao ili kuleta maendeleo kwa kila mwananchi.

"Niwahakikishie Kenya dhamira yetu ya dhati ni kufanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu zaidi katika kuleta maendeleo ya pamoja ya kijamii na kiuchumi baina ya nchi zetu na ukanda wote wa Afrika Mashariki," alisema na kuongeza:

"Tunamwomba Mungu amwezeshe ndugu yetu Ruto pamoja na serikali atakayoiunda, awatie nguvu ili kutumikia vyema nchi hii katika kiwango kinachotarajiwa na wananchi wa Kenya."

**MARAIS WENGINE**

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni alimpongeza Rais anayemaliza muda wake na anayeingia madarakani, huku akisisitiza kuwa katika majadiliano yanayofanyika ushirikiano wa Afrika Mashariki uwe sehemu ya mijadala hiyo.

**Leo 'jana' jioni nimepokea simu kutoka kwa Dk. Ruto akinialika kwenye sherehe ya kuapishwa kwake itakayofanyika hapo kesho (jana). Nasikitika kuwa sitaweza kuhudhuria sherehe hiyo kwa sababu niko nje ya nchi na pia kwa sababu zingine.**

Rais wa Burundi, Évariste Ndayishimiye, aliwapongeza Wakenya kwa kuonyesha ukomavu mkubwa wa kidemokrasia katika uchaguzi uliofanyika nchini humo, huku akiahidi kushirikiana na Rais Ruto kuendeleza ukanda wa Afrika Mashariki.

**ODINGA AKATAA MWALIKO**

Ilielezwa kuwa kiongozi wa Azimio la Umoja, Raila Odinga, aliyechuana na Ruto katika uchaguzi uliomalizika mwezi uliopita, alikataa kuhudhuria sherehe ya kuapishwa kwa Ruto.

Kwa mujibu wa ujumbe uliotolewa jana kwenye mtandao wa Odinga, alisema Rais Ruto alimwalika kwenye hafla hiyo lakini alisema hatakanyaga Kasarani.

"Leo 'jana' jioni nimepokea simu kutoka kwa Dk. Ruto akinialika kwenye sherehe ya kuapishwa kwake itakayofanyika hapo kesho (jana). Nasikitika kuwa sitaweza kuhudhuria sherehe hiyo kwa sababu niko nje ya nchi na pia kwa sababu zingine," alisema.

Odinga aliongeza kwa kukosoa matokeo ya uchaguzi yaliyotolewa na IEBC, ambayo yalimtangaza Ruto kuwa mshindi.

"Kwanza ninaamini kuwa IEBC ambayo ina wajibu wa kufanya uchaguzi nchini, haikufanya uchaguzi huru na wa haki," alisema.

Pia alisema uamuzi wa Mahakama ya Upeo katika kesi ya kupinga ushindi wa Ruto ulikosa kuangazia ushahidi ambao kikosi chake cha mawakili kiliweka mezani.

"La pili ni kwa sababu naamini kuwa maamuzi (uamuzi) yalitolewa (uliotolewa) na mahakama hayakuangazia (hayakuzingatia) sheria na ushahidi hata kama tulikubali," alisema.

Aidha, aliahidi kutoa mwelekeo kwa wafuasi wake mara tu atakaporudi nchini humo akisema ni wazi kwamba bado kuna mengi ya kupiganiwa.

**VIZINGITI ALIVYORUKA RUTO**

Juzi, akizungumza kanisani, Dk. Ruto alisema ushindi wake haukuwa rahisi kutokana na vikwazo vilivyokuwapo na kwamba aliupata kupitia maombi.

Kwa mujibu wa Ruto, vikwazo hivyo ni serikali ya aliyekuwa Rais wa taifa hilo, Kenyatta kuungana na mrengo wa Odinga kushindana naye.Pia machifu na makamishna kote nchini kuagizwa wafanye kampeni dhidi ya mrengo wa Kenya Kwanza na kwamba mawaziri, makatibu wakuu, makamishna na machifu walikuwa wakiwapinga.

Aidha, alisema kura za maoni ambazo zilikuwa zikikarabatiwa ili kuonyesha kwamba hatafaulu kuingia Ikulu na simulizi zilizokuwapo kuwa hakuna naibu rais anaweza kufaulu kuingia Ikulu.

"Huu ushindi hatungepata bila Mungu. Mambo ya binadamu wote yalikuwa kinyume na sisi. Hata tukaambiwa hakuna naibu wa rais ambaye amewahi kuchaguliwa kwa mara ya kwanza, tukaambiwa hakuna rais amechaguliwa akiwa amejaribu mara ya kwanza," alisema.

**VIONGOZI WAHUDHURIA**

Licha ya Rais Samia, Museveni na Ndayisimiye kuhudhuria, viongozi mbalimbali, wakiwamo wakuu wa nchi kutoka mataifa ya Afrika walihudhuria sherehe hizo za uapisho zilizokuwa na shamrashamra ya kila namna.

Marais wengine waliohudhuria na nchi zao kwenye mabano ni Hassan Mohamud (Somalia), Dk. Lazarus Chakwera (Malawi), Umaro Embalo (guinea Bissau), Azali Assoumani (Comoro), Felix Thisekedi (Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo), Julius Maada Bio (Sierra Leone) na Salva Kiir wa Sudan Kusini.

Baada ya Ruto kuapishwa, Rais mstaafu Kenyatta alimkabidhi katiba ya Kenya na kitara cha kijeshi ambacho kinaashiria uhamisho wa mamlaka, udhibiti wa nchi na ulinzi wake ambacho pia kinampa uhalali wa kuwa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

Pia wimbo wa taifa hilo uliimbwa ukiambatana na tukio la kushushwa kwa bendera ya aliyekuwa Rais wa Kenya Kenyatta kuashiria mwisho wa enzi na kisha kupandishwa upya kuashiria enzi mpya. Ruto pia alipigiwa mizinga 21.

Wasanii mbalimbali walisherehesha hafla hiyo kwa nyimbo mbalimbali za dini na za kawaida huku bendi maarufu ya Maroon Commandos ikitumbuiza.

**WATANO WAJERUHIWA**

Katika sherehe hiyo watu watano walijeruhiwa kutokana na kukanyagana na wanaendelea na matibabu katika hospitali mbalimbali.

HABARI MICHEZO

# KOCHA MPYA WA COASTAL KUANZIA ALIPOISHIA MGUNDA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu mpya wa Coastal Union ambaye alitangazwa juzi usiku, Yusuph Chipo, amesema ataanzia pale alipoishia kocha aliyepita, Juma Mgunda ambaye ametimkia Klabu ya Simba ili kuiletea mafanikio timu hiyo.

Akizungumza baada ya kutambulishwa rasmi, kocha huyo raia wa Kenya, alisema kwa kushirikiana na uongozi na kamati, anaamini kuwa wataifanya Coastal Union kuendelea kuwa timu shindani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Sisi kama benchi la ufundi tutashirikiana na uongozi na wachezaji na kamati zilizopo kuipatia Coastal inachokihitaji, namshukuru sana Kocha Mgunda kwa kuweka msingi mkubwa kwenye kikosi hiki, na mimi ninaanzia pale alipoachia kocha huyo," alisema kocha huyo ambaye aliwahi kuhudumu kwenye timu hiyo.

**Ofisa habari wa klabu hiyo, Miraji Wandi, alisema kuondoka kwa Mgunda kuliwafanya viongozi wa klabu hiyo kukaa na kuangalia nani anaweza kurithi mikoba yake na kwa kushirikiana na Kamati ya Usajili na Kamati ya Utendaji, ukaona ni wakati sahihi wa kumchukua Chipo.**

Wakati huo huo, klabu ya Pamba imedai kupokea maombi kutoka kwa mwalimu Chipo ya kuvunja mkataba wake wa mwaka mmoja ili kujiunga na Coastal Union na kueleza wameridhia.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, imesema baada ya majadiliano ya wapande zote mbili wamefikia makubaliano hayo, na kukubali ombi lake la kutaka kujiunga na timu hiyo ya Ligi Kuu, hivyo kuvunja mkataba.

Pamba ambayo iko kwenye Ligi ya Championship, imesema wakati mchakato wa kutafuta kocha mpya unaendelea, timu itakuwa chini ya Stephen Matata na kuwataka mashabiki wake kuwa watulivu.

MILIKI...



Mchezaji wa Timu ya Pan Africans, Allen Matius, akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa KMC FC katika mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. KMC ilishinda mabao 5-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tanzania yang'ara michuano SARPCCO*

**Saada Akida na Camila Bonanza** (TUDARCo)

TIMU za Tanzania zimefanya vizuri kwenye Michezo ya Shirikisho la Jumuiya ya Majeshi ya Polisi ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SARPCCO GAMES), ambapo timu ya riadha ikiongoza kwa kupata medali za dhahabu 16, shaba 12 na fedha saba.

Timu zingine ni ya Netiboli ambayo juzi iliibuka na ushindi wa magoli 37-35 dhidi ya Namibia, huku kwenye mchezo wa Vishale (Darts) kwa upande wa wanawake na wanaume zikiingia nusu fainali wakati Volleyball na mpira wa miguu kwa wanaume zikitinga hatua ya robo fainali.

Mashindano hayo ambayo yalianza kutimua vumbi tangu Septemba 3, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Uhuru, JK Park, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Gwambina huku yakishirikisha nchi za Afrika Kusini, Angola, DRC Kongo, Eswatini, Lesotho, Malawi, Msumbiji, Namibia, Shelisheli, Zambia, Zimbabwe na mwenyeji Tanzania, yatafikia tamati keshokutwa, Ijumaa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Kitengo cha Michezo cha Jeshi la Polisi pia Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Jonas Mahanga, alisema tangu mashindano yalipoanza timu za Tanzania zinazoshiriki michezo yote zinafanya vizuri.

Alisema riadha inaongoza hadi sasa ikiwa na jumla ya medali 40 na mpira soka kwa wanaume wameingia hatua ya robo fainali, na kwamba kitendo cha kufika hatua hiyo ni mafanikio makubwa kwao.

"Kwa matokeo haya na kufanya vizuri kwa timu zetu, tunatarajia baadhi ya michezo pia kuibuka na ubingwa licha ya kuwapo kwa ushindani mkubwa kutoka kwa mataifa mengine yanayoshiriki mashindano haya.

"Kwa ujumla katika mashindano haya, makocha wa timu za Tanzania wamepata mwanga wa kuona udhaifu na ubora wa timu zetu kuelekea kujiandaa na mashindano mengine yaliyopo mbele yetu hapo baadaye," alisema Mahanga.

Alisema baada ya michuano hiyo kufikia tamati Ijumaa wiki hii, timu zote zitaendelea na kambi kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya Majeshi Tanzania yanayotarajiwa kufanyika Oktoba 7 hadi 12, mwaka huu, jijini Mbeya.

"Pia Novemba 14 hadi 21, mwaka huu, tutakuwa na mashindano ya Afrika Mashariki yatakayofanyika Kigali nchini Rwanda, kwa hali hiyo, michuano ya SARPCCO inatusaidia kwa ajili ya mashindano hayo," alisema Mahanga.

## Uwanja wa kisasa Dodoma kujengwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema mipango ya ujenzi wa uwanja mpya wa soka Dodoma bado upo pale pale baada ya kufuatilia utekelezaji wa ahadi iliyotolewa na Mfalme wa Morocco.

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul, ndiye aliyetoa kauli hiyo bungeni jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Morogoro Kusini (CCM), Innocent Kalogeris, ambaye alitaka kujua ni lini ahadi ya ujenzi wa uwanja huo iliyotolewa na Mfalme wa Morocco itatekelezwa.

Aidha, Gekul alisema katika kuhakikisha kwamba mradi huo unatekelezwa serikali imedhamiria kutafuta fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali vikiwamo sekta binafsi na wabia wa maendeleo.

"Mawasiliano kuhusu utekelezaji wa mradi huo baina ya Serikali ya Tanzania na Morocco bado yanaendelea,"alisema.

## Gofu Wanawake waigeukia serikali

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Gofu ya Wanawake, Hawa Wanyeche, ameiomba serikali iwape sapoti mara kwa mara ili wazidi kufanya vizuri ikiwamo kuitangaza vema Tanzania kwenye michuano ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Wanyeche alisema amegundua timu ambazo zilikuwa hapa nchini na kufanya vizuri kwenye mashindano ya All Africans Challenge Trophy, yaliyomalizika hivi karibuni, wamepata sapoti kubwa kutoka serikali zao.

"Tunaishukuru serikali kwa msaada mkubwa iliyotupa kwenye mashindano yaliyopita, tunaomba iwe inatusapoti mara kwa mara, wenzetu wanawezeshwa na serikali zao ili kufikia mafanikio," alisema Wanyeche.

Aidha, aliwataka wanawake kujitokeza kujiunga na mchezo huo kuliko kukaa kizembe bila mazoezi.

"Ninashauri wanawake wezangu wa Tanzania kujitokeze kujiunga na mchezo huu, waache kukaa bila kufanya mazoezi," alisema nahodha huyo.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO KAKATAA MAMILIONI

CRISTIANO Ronaldo alikataa mshahara wa pauni milioni 211 kwa mwaka kuichezea klabu ambayo haijatajwa nchini Saudi Arabia, lakini sasa mchezaji huyo wa Manchester United mwenye umri wa miaka 37, raia wa Ureno anaifikiria ofa hiyo. ***(Athletic via Mirror)***

### KANE AITAKA BAYERN

HARRY Kane mwenye umri wa miaka 29, anashawishika kukata kuichezea Bayern Munich, huku kukiwa na mawasiliano na mabingwa hao wa Ujerumani. ***(Express)***

### WATANO KUONDOKA UNITED

WACHEZAJI Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 24, Luke Shaw (27), David de Gea (31) na Diogo Dalot (23) pamoja na Fred (29), wanaweza kuondoka Manchester United kama wachezaji huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

### AKANJI AIFUNGUKIA UNITED

MLINZI wa kati mpya wa Manchester City, Manuel Akanji mwenye umri wa miaka 27, ambaye amejiunga na Borussia Dortmund kwa ada ya pauni milioni 15, amebainisha kwamba alikuwa shabiki wa Manchester United wakati akiwa mdogo. ***(Blick)***

### GAVI KUJIFUNGA BARCA

KIUNGO wa Hispania Gavi anaweza kusaini mkataba mpya na Barcelona wiki hii ambapo kutakuwa na kipengele cha kumuuza kwa euro bilioni moja mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, ambaye amekuwa akihuishwa na Liverpool. ***(Diario Sport)***

### UNITED WAKOMAA NA JONG

KLABU ya Manchester United inaamini nafasi ya kumsajili kiungo wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, ipo na wapo tayari kutoa pauni milioni 73. ***(Mirror)***

### NUNEZ KASTAHILI LIVER

RAIS wa Benfica, Rui Costa anaamini kiasi cha pauni milioni 64 kilichotolewa na Liverpool kwa Darwin Nunez kilikuwa sahihi kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Mail)***

### ORIGI USAJILI MBAYA

STRAIKA wa Ubelgiji, Divock Origi, 27, ambaye aljiunga na AC Milan kama mchezaji huru kutoka Liverpool Julai, mwaka huu ni usajili mbaya zaidi kwa klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. ***(Mail)***

### HENRY AMSIFIA BALOGUN

THIERRY Henry amesifia uamuzi wa Folarin Balogun mwenye umri wa miaka 21, kujiunga na Reims kwa mkopo kutoka Arsenal. ***(Evening Standard)***

### MARQUINHOS KWA MKOPO

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anataka kumpeleka kwa mkopo winga wa Brazil, Marquinhos mwenye umri wa miaka 19. ***(FourFourTwo)***

### GVARDIOL KATAJWA CHELSEA

KLABU ya RB Leipzig ilikataa ofa ya Chelsea kumsajili mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol, 20. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# N'GOLO ATAKA MKATABA MREFU KUBAKI CHELSEA

**LONDON,** England

**Bado hakuna ofa rasmi, huku klabu na mchezaji huyo sasa wakifanyia kazi kile ambacho kila...**

N'GOLO Kante ameifahamisha Chelsea kwamba, anataka kujitolea kwa muda mrefu kwa 'Blues' hao kama atasaini mkataba mpya, kwa mujibu wa 90min.

**Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 31, amengia mwaka wa mwisho wa mkataba wake pale Stamford Bridge na Chelsea wanataka kushughulikia mustakabali wa mchezaji huyo ambaye bado anaonekana kuwa mmoja wa viungo bora zaidi duniani anapokuwa fiti.**

Mazungumzo ya awali kuhusu kuongezwa kwa muda yamefanyika na 90min inaelewa kuwa Kante ameweka wazi kwamba anataka kujitolea kwa miaka mitatu kutoka kwa Chelsea, ambayo utawala wao wa awali ulikuwa na wasiwasi kuhusu kuwapa mikataba mirefu wachezaji wanaozeeka.

Bado hakuna ofa rasmi, huku Chelsea na Kante sasa wakifanyia kazi kile ambacho kila mmoja anaonekana kukitaka.

Jambo moja ambalo Chelsea wanapaswa kuzingatia ni rekodi ya hivi majuzi ya majeraha ya Kante.

Mfaransa huyo amekosa mechi tano za mwisho za timu yake katika michuano yote kutokana na tatizo la misuli.

Zaidi ya hayo, mustakabali wa Kante unahusishwa na ule wa kiungo mwenzake Jorginho, ambaye atafikisha umri wa miaka 31, Desemba na pia yuko katika miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake wa sasa.

Mazungumzo bado hayajafanyika na Muitaliano huyo, ambaye amezivutia klabu nyingi kutoka Serie A, kuwa kuna uwezekano kwamba Chelsea itawapa Jorginho na Kante mikabati mpya.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,031,2

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 14 NA 15 SEPTEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/09/22 | 19:45 | Shakhtar Donetsk vs Celtic | 3.05 | 3.50 | 2.24 |
| 02. 14/09/22 | 22:30 | Colon Santa Fe vs San Lorenzo | 2.32 | 2.99 | 2.99 |
| 03. 15/09/22 | 00:00 | Everton Vina del Mar vs Nublense | 2.29 | 3.04 | 2.99 |
| 04. 15/09/22 | 03:05 | Alebrijes De Oaxaca vs CF Atlante | 2.89 | 3.09 | 2.32 |
| 05. 15/09/22 | 03:30 | Lanus vs Boca Juniors | 2.85 | 2.99 | 2.41 |
| 06. 15/09/22 | 05:00 | Vancouver Whitecaps vs LA Galaxy | 2.52 | 3.61 | 2.59 |
| 07. 15/09/22 | 19:45 | Olympiakos vs SC Freiburg | 2.58 | 3.39 | 2.58 |
| 08. 15/09/22 | 19:45 | Karabakh vs Nantes | 2.54 | 3.30 | 2.69 |
| 09. 15/09/22 | 19:45 | Djurgardens IF vs Molde | 2.40 | 3.30 | 2.86 |
| 10. 15/09/22 | 22:00 | Basaksehir vs Fiorentina | 2.73 | 3.28 | 2.51 |
| 11. 15/09/22 | 22:00 | Steaua Bucuresti vs Anderlecht | 2.72 | 3.32 | 2.50 |
| 12. 15/09/22 | 22:00 | Rigas Futbola Skola vs Hearts | 2.68 | 3.24 | 2.58 |
| 13. 15/09/22 | 22:00 | Partizan vs Nice | 2.72 | 3.37 | 2.47 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CONTE KUMPUMZISHA SON



**LONDON,** England

KOCHA Antonio Conte anaamini kuwa itakuwa bora zaidi ikiwa Tottenham Hotspur itaweza kumpumzisha Son Heung-min badala ya mshambuliaji huyo nyota kucheza katika kila mechi.

Son amecheza angalau mechi 40 kwenye mashindano yote katika kila msimu kwa misimu saba kamili akiwa Spurs, wakati katika kampeni yake ya kwanza tu nchini Uingereza alianza chini ya mechi 30.


Msimu huu, mshambuliaji huyo wa Korea Kusini ameanza mechi zote saba za klabu yake, ingawa bado hajafunga na ametoa pasi moja pekee. Huku Richarlison akisajiliwa mwishoni mwa msimu, kufuatia ujio wa Januari wa Dejan Kulusevski, Conte anaonekana sasa kutaka kumwacha Son nje ya timu yake kutokana na kiwango kidogo.

Akizungumzia kuweka pamoja Son, Richarlison, Kulusevski na Harry Kane kwenye kikosi cha kwanza, Conte alisema: "Mechi iliyoahirishwa inaniruhusu kufanya uamuzi tofauti.

"Dhidi ya Man City, ningecheza na wachezaji fulani, lakini sasa ninabadilisha mambo katika akili yangu." "Nadhani unapojaribu kujenga kitu muhimu, kwa matamanio na kujaribu kuwa mshindani na kushinda, lazima ubadilishe tabia za zamani.

"Kwa sababu hii, wachezaji wote wanapaswa kukubali kwamba mzunguko ni sehemu ya kipengele hiki. Tuna wachezaji wanne mbele, na ni vigumu sana hivi sasa kuacha mmoja.

"Lazima nichukue uamuzi bora, wakati mwingine kwa wachezaji. Wakati mwingine ni bora kuingia kwa dakika 20, 30 kwa ajili yao.



## *Kounde afunguka kutua Man City*

**BARCELONA,** Hispania

MLINZI wa Barcelona, Jules Kounde amedai nusura asaini Manchester City miaka miwili iliyopita baada ya mazungumzo na Kocha Pep Guardiola.

Mfaransa huyo alijiunga na Barcelona kutoka Sevilla msimu huu wa majira ya joto kwa dili la thamani ya euro milioni 53.

Chelsea walihusishwa sana, lakini hawakuweza kuafikiana kuhusu ada na Sevilla.

Kounde sasa amethibitisha kwamba, Man City ilifanya majaribio ya kumsajili mwaka mmoja kabla.

Alipoulizwa na El Pais kama tetesi za Guardiola kujaribu kumsajili kule Man City zilikuwa za kweli, Kounde alisema: "Ndiyo, katika mwaka wangu wa kwanza Sevilla, aliniita. Aliniambia kwamba ananipenda na alifikiri ningefaa kucheza chini yake."

Hatimaye Kounde alipata uhamisho wake mkubwa msimu uliopita wa majira ya joto, chini ya Kocha wa Barcelona, Xavi Hernandez.

Mfaransa huyo, hata hivyo, alisema kuna mambo mengi yanayofanana kati ya Xavi na Guardiola.

## HABARI MICHEZO

243,893/-

# MKAZI KAHAMA ALAMBA MILIONI 5.3/- ZA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Shinyanga wilayani Kahama, Paulo Method, ameshinda kiasi cha Sh. 5,362,400 ikiwa ni Bonasi ya Jackpot ya SportPesa iliyochezwa mwishoni mwa wiki baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya 13.

**Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya hundi katika ofisi za SportPesa jijini Dar es Salaam jana, Paulo alisema alianza kucheza na SportPesa miaka minne iliyopita.**

"Nilianza kucheza na SportPesa mwaka 2018 baada ya aliyekuwa mwalimu wangu, Leonard ambaye ni wakala wa Airtel Money, Halopesa na M-pesa, kunifundisha kucheza," alisema.

Method alisema, alivutiwa na SportPesa baada ya kuona kiwango cha bonasi zake ni kikubwa kuliko makampuni mengine.

"Mimi nilikuwa napenda kucheza hii michezo ya 'tusua mapene'. Sasa siku moja nilikutana na mwalimu aliyenifundisha kuanzia form one (kidato cha kwanza mpaka form four (kidato cha nne). Aliponiona ninaweka pesa kwa ajili ya michezo hiyo akaniambia mdogo wangu kwa nini hauchezi na SportPesa, nikamjibu sijui, ndipo alipoanza kunifundisha.

"Kwa ufupi mwanzo ulikuwa mgumu kidogo, ila namshukuru Mungu baada ya muda niliweza kucheza mwenyewe kwa urahisi na bahati nzuri niliwahi kushinda Sh. milioni 10 kwenye Bonasi ya Jackpot ya timu 13," alisema.

Akielezea namna alivyopata ushindi huu wa Supa Jackpot Bonus, alisema aliweka mkeka wake siku ya Ijumaa na baadaye kusubiria matokeo kuanzia Jumamosi ambapo timu zote alizozibetia zilimpa matokeo.

Aidha, Method aliwashauri Watanzania wasisite kucheza kwa wingi kwani Supa Jackpot ya SportPesa imeboreshwa na kukupa unafuu katika uchaguzi ucheze Jackpot yenye timu ngapi.

Kushusu matumizi ya fedha alizoshinda, alisema atawekeza kwenye makazi yake ambayo anajenga na pia kidogo kitakachobaki ataongezea mtaji kwenye biashara yake.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya, alimpongeza Method kwa ushindi wake na kuwaasa Watanzania waendelee kuiamini na kucheza na SportPesa kwani wanaweza kushinda kama Method. "Niwakumbushe tu Watanzania Supa Jackpot kwa wiki hii ni Sh. 1,031,243,893, endeleeni kucheza mshinde kama Paulo," alisema.




Mshindi wa Jackpot Bonasi, Paul Method kutoka Kahama mkoani Shinyanga, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 5.3 baada ya kukabidhiwa juzi, kutokana na kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. Jackpot ya SportPesa kwa wiki hii ni Shilingi 1,031,243,893. **MPIGAPICHA WETU**

# *Bares aanza vema Mlandege Ligi Z'bar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mohamed Abdallah 'Bares' ameanza vema mechi yake ya kwanza akiwa Kocha Mkuu wa timu ya Mlandege FC, baada ya kuachana na JKT Tanzania.

Mlandege FC ikiwa chini ya Bares, juzi iliibuka na ushindi wake wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kuichapa Black Sailor bao 1-0 katika mchezo wa ligi hiyo uliopigwa Uwanja wa Amaan majira ya saa 10 jioni.

Bao pekee la Mlandege FC, lilipachikwa nyavuni na mshambuliaji Abdulnassir Asaa 'Gamal'katika dakika ya 60.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Bares alisema kwa sasa ana mipango mingi ya kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar kwa kuifanya kucheza vizuri na kwa mipango ili nafasi wanazozipata waweze kuzigeuza kuwa mabao.

Alisema hilo linawezekana kwa kuwa timu hiyo ina wachezaji wazuri na ni vijana, hivyo inakuwa kazi rahisi kuwafundisha namna bora ya uchezaji na kufanya vizuri zaidi.

Akizungumzia mchezo huo dhidi ya Black Sailor, alisema mchezo huo ulikuwa mgumu katika dakika zote na wapinzani wao walicheza vizuri kwa kuwa timu zote zina wachezaji vijana.

Alisema wachezaji walifanya kazi kubwa kulilinda goli lao licha ya kuandamwa na mashambulizi makali hasa katika dakika za mwisho za mchezo.

Mlandege FC itashuka tena dimbani Jumapili wiki hii dhidi ya mpinzani wake mkubwa, Malindi FC,

Katika matokeo mengine ya ligi hiyo, Zimamoto FC ilishindwa kutamba dhidi ya Maafande wa JKU kwa kutoka sare tasa kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Amaan majira ya saa moja usiku.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/09/22 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.73 | 3.33 | 2.48 |
| 02. 17/09/22 | 19:00 | Spezia vs Sampdoria | 2.55 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 17/09/22 | 19:15 | Zulte Waregem vs St. Truiden | 2.94 | 3.49 | 2.28 |
| 04. 17/09/22 | 19:30 | Valencia vs Celta Vigo | 2.35 | 3.08 | 3.18 |
| 05. 17/09/22 | 19:30 | Borussia Monchengladbach vs RB Leipzig | 2.93 | 3.57 | 2.23 |
| 06. 17/09/22 | 20:00 | PAU F vs Valenciennes | 2.72 | 3.07 | 2.77 |
| 07. 17/09/22 | 20:00 | Bastia vs Metz | 2.52 | 3.17 | 2.92 |
| 08. 17/09/22 | 20:00 | US Quevilly Rouen vs Laval | 2.47 | 3.16 | 3.01 |
| 09. 17/09/22 | 22:30 | Atlanta United vs Philadelphia Union | 2.30 | 3.61 | 2.91 |
| 10. 18/09/22 | 02:30 | New England Revolution vs Montreal Impact | 2.35 | 3.57 | 2.87 |
| 11. 18/09/22 | 13:15 | GO Ahead Eagles vs FC Emmen | 2.36 | 3.48 | 2.83 |
| 12. 18/09/22 | 14:30 | Jahn Regensburg vs St. Pauli | 2.88 | 3.62 | 2.26 |
| 13. 18/09/22 | 15:00 | Randers FC vs Silkeborg IF | 2.47 | 3.39 | 2.74 |
| 14. 18/09/22 | 15:30 | SC Heerenveen vs Twente | 2.73 | 3.58 | 2.38 |
| 15. 18/09/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Troyes | 2.40 | 3.33 | 2.83 |
| 16. 18/09/22 | 17:30 | FC Arouca vs Vitoria Guimaraes | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 17. 18/09/22 | 19:00 | FC Midtjylland vs FC Copenhagen | 2.50 | 3.40 | 2.70 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 14/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2105 | Montedio Yamagata vs Yokohama | 2.35 | 3.15 | 2.80 |
| 13:00 | 2488 | Ansan Greeners vs Jeonnam Dragons | 2.70 | 3.34 | 2.33 |
| 13:00 | 4329 | Vissel Kobe vs FC Tokyo | 2.18 | 3.25 | 3.00 |
| 13:00 | 4560 | Tokyo Verdy vs Blaublitz Akita | 1.84 | 3.19 | 4.13 |
| 13:00 | 4567 | Incheon Utd vs Ulsan Hyundai | 4.41 | 3.48 | 1.71 |
| 13:00 | 5320 | Tochigi SC vs Vegalta Sendai | 3.05 | 2.95 | 2.31 |
| 13:00 | 5805 | Jeonbuk Hyundai vs Seongnam Ilhwa | 1.44 | 4.24 | 5.91 |
| 13:30 | 1589 | Seoul E Land vs Chungnam Asan | 2.79 | 3.09 | 2.39 |
| 13:30 | 2138 | Nagoya Grampus vs Kawasaki Frontale | 3.54 | 3.14 | 2.00 |
| 13:30 | 3550 | Ventforet Kofu vs Niigata Albirex | 3.14 | 3.19 | 2.14 |
| 13:30 | 4719 | Anyang vs Gwangju | 2.85 | 3.19 | 2.30 |
| 14:00 | 2696 | Bangkok Glass vs Port FC | 1.73 | 3.57 | 4.11 |
| 15:00 | 2146 | Lokomotiv Moscow vs FC Krasnodar | 2.46 | 3.39 | 2.51 |
| 15:00 | 5659 | Sochi vs Torpedo Moscow | 1.35 | 4.50 | 7.25 |
| 16:00 | 1316 | Tanzania Prisons vs Simba | 4.62 | 3.14 | 1.77 |
| 16:00 | 3026 | Astana vs Tobol Kostanay | 1.73 | 3.58 | 4.12 |
| 16:00 | 5034 | Kedah vs Selangor FC | 1.84 | 3.64 | 3.54 |
| 16:30 | 3564 | Tunari vs Dinamo Bucuresti | 4.13 | 3.54 | 1.74 |
| 17:00 | 3138 | SKF Sered vs Raca Bratislava | 2.55 | 3.83 | 2.24 |
| 17:00 | 5776 | Sloboda Tuzla vs Velez Mostar | 2.38 | 2.85 | 3.05 |
| 17:30 | 2922 | Kryliya Sovetov vs Zenit St Petersburg | 4.23 | 3.93 | 1.64 |
| 17:30 | 2990 | CSKA Moscow vs Ural Yekaterinburg | 1.39 | 4.13 | 7.28 |
| 17:30 | 3464 | Hajduk Split vs HNK Rijeka | 1.41 | 4.41 | 6.08 |
| 17:30 | 5679 | Rostov vs Gazovik Orenburg | 1.41 | 4.22 | 6.47 |
| 18:00 | 5070 | Aktobe vs Taraz | 1.55 | 3.87 | 5.10 |
| 18:05 | 3966 | Al-Shamal vs Al Ahli Doha SC | 2.22 | 3.50 | 2.76 |
| 19:00 | 3538 | Kapa vs KuPS Akatemia | 1.46 | 4.73 | 4.93 |
| 19:45 | 2843 | Shakhtar Donetsk vs Celtic | 3.06 | 3.41 | 2.18 |
| 19:45 | 5063 | AC Milan vs Dinamo Zagreb | 1.23 | 5.61 | 11.03 |
| 20:00 | 2231 | FSV Frankfurt vs SSV Ulm | 4.33 | 3.84 | 1.64 |
| 20:00 | 2950 | Aldosivi vs NewellS Old Boys | 2.90 | 3.09 | 2.32 |
| 20:15 | 4550 | Qatar SC vs Al Rayyan SC | 2.50 | 3.24 | 2.55 |
| 21:30 | 2190 | Union Espanola vs La Serena | 1.65 | 3.63 | 4.61 |
| 21:30 | 5729 | Monopoli vs Avellino | 2.82 | 2.82 | 2.77 |
| 21:45 | 1367 | Millwall vs QPR | 2.25 | 3.19 | 3.09 |
| 21:45 | 2456 | Rotherham vs Blackpool | 2.28 | 3.25 | 3.00 |
| 21:45 | 2752 | Luton Town vs Coventry | 2.11 | 3.35 | 3.25 |
| 21:45 | 3688 | Norwich City vs Bristol City | 1.64 | 3.84 | 4.79 |
| 22:00 | 1359 | Maccabi Haifa vs Paris St Germain | 12.24 | 6.82 | 1.17 |
| 22:00 | 1494 | Reading vs Sunderland | 2.55 | 3.21 | 2.65 |
| 22:00 | 1669 | Real Madrid vs RB Leipzig | 1.53 | 4.40 | 5.00 |
| 22:00 | 2274 | Copenhagen vs Sevilla FC | 3.44 | 3.34 | 2.04 |
| 22:00 | 2960 | West Bromwich vs Birmingham | 1.42 | 4.30 | 7.00 |
| 22:00 | 3988 | Juventus vs Benfica | 2.26 | 3.22 | 3.07 |
| 22:00 | 4019 | Pescara Calcio vs Crotone | 2.27 | 3.13 | 3.23 |
| 22:00 | 4805 | Rangers vs Napoli | 3.91 | 3.71 | 1.80 |
| 22:00 | 5371 | Manchester City vs Borussia Dortmund | 1.21 | 6.18 | 10.59 |
| 22:00 | 5737 | Chelsea vs RB Salzburg | 1.32 | 5.18 | 7.57 |
| 23:00 | 4695 | Cobresal vs Colo Colo | 3.10 | 3.24 | 2.13 |
| 23:45 | 5858 | Libertad Asuncion vs Tacuary Asuncion | 1.36 | 4.52 | 7.07 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Septemba 14, 2022

Nipashe



Conte kumpumzisha Son UKURASA 22

# Simba bila Kanoute yaipania Prisons leo

●●● Ni mechi ya kisasi, wenyewe wasema njoo tupo tayari, Onyango naye atajwa...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha Simba kilichosafiri kwa ndege jana asubuhi, leo jioni kikitarajia kushuka Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya kucheza dhidi ya Tanzania Prisons kwenye mechi ya raundi ya nne ya Ligi Kuu Tanzania Bara, kitawakosa nyota wake wawili viungo, Sadio Kanoute na Victor Akpan, imeelezwa.

**Simba itashuka uwanjani leo ikitaka kuendeleza moto wao wa kushinda ugenini baada ya kutoka kushinda mabao 2-0 dhidi ya Nyasa Big Bullets nchini Malawi, lakini ikiwa na kumbukumbu mbaya ya kupoteza kwa bao 1-0 msimu uliopita uwanjani hapo dhidi ya Prisons.**

Juni 26, mwaka huu, Ligi Kuu msimu uliopita, Simba ikiwa na Kocha Mkuu, Didier Gomes ilifungwa bao 1-0, lakini haikuweza kupata pointi yoyote ikiwa kwenye uwanja huo, kwani ilipoteza pia kwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City.

Simba ambayo kabla ya mechi za jana, ilikuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi saba sawa na Mtibwa Sugar, Yanga na Singida Big Stars, mechi iliyopita ya Ligi Kuu ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMC FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema Akpan na Kanoute watakosa mchezo huo kutokana na sababu tofauti huku Shomari Kapombe akitarajiwa kuwa miongoni mwa kikosi kitakachoivaa Prisons.

"Kikosi chetu kipo vizuri, wachezaji wamefanya mazoezi leo (jana) katika uwanja wetu wa Bunju, mazoezi yaliendelea vizuri tayari kwa ajili ya mchezo wetu wa kesho dhidi ya Prisons na kikosi kitaondoka leo (jana) saa 12 jioni.

"Kuna baadhi ya wachezaji watakosa mchezo huo, akiwamo Akpan ambaye ni majeruhi, huku Kanoute akiwa na kadi tatu za njano, hivyo hawezi kucheza mchezo huo, lakini Kapombe yupo vizuri, amerudi na katika mechi ya kesho (leo) kocha anaweza kumtumia, pia Gadiel Michael bado hayupo sawa," alisema Ahmed.

Aidha, Ahmed alisema pamoja na nyota hao kuukosa mchezo huo, habari njema ni kwamba beki wao, Joash Onyango amerejea kikosini kwa ajili ya kukitumikia kikosi hicho kwenye mechi za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa upande wa Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema: "Muda ni mfupi tangu tulipotoka Malawi na kujiandaa na mechi hii, lakini tupo tayari na itakuwa mechi nzuri".

Kwa upande wa wenyeji wa mchezo huo, Prisons wamesema wako tayari kuikabili Simba licha ya kutambua utakuwa mchezo mgumu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Enock Mwanguku, alisema: "Tutaingia kwa heshima zote kwa kuiheshimu Simba kwani ni timu kubwa na ina historia kubwa katika soka la Tanzania, na sisi pia tumejipanga vema kwani hali ya timu iko vizuri."

Aidha, alisema wao kama timu kwa sasa hawaangalii historia ya nyuma kwa kuwa msimu uliopita hawakumaliza vizuri, lakini kwa msimu huu wamesahau ya nyuma na wako katika kuandika historia mpya.

***Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Hadija Mngwai na Joram Gervas (TUDARCo)***

TUPO TAYARI...



Mfumaniaji nyavu hatari wa Simba, Moses Phiri (kulia), wakipasha pamoja na beki wa kushoto wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala'. Wachezaji hao wanatarajiwa kushuka Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya leo wakati wakiivaa Tanzania Prisons kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: SIMBA**

# Tshabalala, Mwamnyeto watemwa Stars, Banda...

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha wachezaji 23 kimeitwa Taifa Stars huku beki Abdi Banda akirejeshwa kikosini kitakachoingia kambini Jumapili wiki hii kwa ajili ya maandalizi ya michezo miwili ya kirafiki dhidi ya Libya, iliyopo katika Kalenda ya Shirikisho la Soka Ulimwenguni (Fifa).

Hata hivyo, mabeki wawili nguli, beki wa pembeni, Mohamed Hussein 'Tshabalala' kutoka Simba na wa kati kutoka Yanga, Bakari Mwamnyeto, hawakujumuishwa katika kikosi hicho kilichopo chini ya Kocha Mrundi Honuor Janza.

Banda anayekipiga katika klabu ya Chippa United ya Afrika Kusini mara ya mwisho kuitwa katika kikosi cha Stars ilikuwa mwaka 2019, ikijiandaa na mechi dhidi ya Burundi katika mchezo wa kirafiki chini ya Kocha Etienne Ndayiragije.

Wachezaji walioitwa ni Aishi Manula, Beno Kakolanya, Mzamiru Yassin na Habib Kyombo (Simba), Saidi Kipao, Datius Peter David Luhende na Abdallah Mfuko (Kagera Sugar), Kibwana Shomari, Dickson Job na Feisal Salum (Yanga).

Wengine ni Abdulmalick Adam na Mohammed Banka (Namungo FC), Abdi Banda (Chippa United), Carlos Protas na Ibrahim Joshua (Tusker FC ya Kenya), Oscar Masai (Geita Gold), Himid Mao (Ghazl El Mahalla-Misri), Sospeter Bajana (Azam FC), David Uromi (Moroka Swallows-Afrika Kusini), Mbwana Samatta (Genk- Ubelgiji), Simon Msuva (Al Qadsiah FC- Saudi Arabia) na Said Khamis (Hatta Club- UAE).

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >